**5 NOVEMBA, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SABA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 5 Novemba, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali.

Waheshimiwa tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimuite Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 88

**Ushuru wa Magari ya Makaa ya Mawe Mtwara, Mikindani**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA K.n.y. MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, Halmashauri ya Mtwara Mikindani ilikusanya kiasi gani cha ushuru wa magari yanayosafirisha Makaa ya Mawe kwa mwaka 2022/2023?

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Tunza Malapo. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuru wa makaa ya mawe katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, Mikindani, hutozwa kwa makaa ya mawe yanayosafirishwa nje ya nchi tu kwa kiwango cha shilingi 20,000 kwa tani 30. Ushuru huo katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, Mikindani, ulianza kutozwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo jumla ya shilingi milioni 754 zimekusanywa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kwa niaba ya Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kutokana na jibu la msingi alilojibu Mheshimiwa Waziri, anasema inatozwa shilingi 20,000 kwa tani 30. Je, fedha hizo zilipangwa wakati gani kwa maana naona thamani yake ni ndogo kulingana na mali ambayo inachukuliwa? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Sisi kama wananchi na watu tunaotoka kwenye majimbo tuna wawekezaji wengi sana katika majimbo yetu. Kwa nini TAMISEMI haitoi mahesabu haya kwenye halmashauri zetu na kutangaza kwa umma, ili wananchi waweze kunufaika na mali hizi. Katika Jimbo la Rungwe tuna kiwanda cha *TOL*, tuna kiwanda cha chai, ni kwa nini Serikali haitoi matangazo ya mapato, ili wananchi wajue wanapata nini pale wawekezaji wanapofanyia kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Halmashauri zetu zina muundo wa kuwa na Vitengo vya Sheria na Baraza la Madiwani kwa hiyo, maamuzi yote ya sheria ndogo za ukusanyaji wa mapato ya

halmashauri zinatungwa na Baraza la Madiwani. Kwa hiyo, kiwango hiki cha shilingi 20,000 kilitungwa na Baraza la Madiwani la Manispaa ya Mtwara Mikindani na kinaendelea kutozwa. Ikiwa itaonekana kiwango hiki hakitoshelezi basi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutalitafakari na kushauri Manispaa ya Mtwara Mikindani, kuona hatua zaidi za maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusiana na kampuni mbalimbali zinazofanya kazi katika halmashauri zetu. Kuna Sheria ya *Cooperate Social Responsibility* (mchango wa jamii kwa kampuni zinazofanya shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo), sheria hiyo inatekelezwa kwa halmashauri zote na ni wajibu wa Mkurugenzi, Menejimenti nzima na Baraza la Madiwani kuhakikisha kwamba wananufaika kwa kufuata sheria hiyo na wanatoa matangazo hayo kwa jamii, ili jamii ijue kwamba inanufaika na utaratibu huo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, naona hamna maswali.

Sasa nimuite Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, aulize swali lake.

Na. 89

**Ujenzi wa Wodi Kituo cha Afya Kintinku**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga *OPD* na wodi za wagonjwa katika Kituo cha Afya Kintinku?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Kintinku ni moja ya vituo vya afya vilivyopokea fedha kiasi cha shilingi milioni 500 za ukarabati katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo fedha hizo zilijenga jengo la wazazi, jengo la upasuaji, maabara, jengo la

kufulia, jengo la kuhifadhia maiti pamoja na nyumba ya mtumishi. Majengo haya yamekamilika na yanatoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya vituo vya afya kwa kujenga miundombinu iliyosalia ikiwemo majengo ya kuhudumia wagonjwa wa nje. Hivyo, Kituo cha Afya cha Kintinku kitaingizwa kwenye mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Nkonko ambacho nacho kilipewa fedha na Serikali kwa ajili ya kujenga jengo la kuhifadhia maiti *(mortuary),* mpaka sasa hivi hakitumiki kwa sababu hakuna jokofu. Je, ni lini Serikali itapeleka jokofu kwa ajili ya kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya cha Nkonko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kata ya Makanda ambayo ipo zaidi ya kilometa 25 haina kituo cha afya, lakini inahudumia kata jirani za Makutupora, Makulu, Makanda B, Bahi na vilevile Kata ya Mpendwa na ni mojawapo ya kata ambayo tuliiweka kwenye kata za kujengewa vituo vya afya vya kimkakati. Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Makanda kama kituo cha afya cha kimkakati? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika kipindi cha mwaka huu wa fedha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetoa zaidi ya shilingi bilioni 250 katika halmashauri zote 184 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manyoni kuweka kipaumbele cha kununua jokofu, kwa ajili ya hicho kituo cha afya ili wananchi wapate huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, Serikali tayari imeshatoa taarifa na maamuzi ambayo kupitia Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, majimbo yote 214 ya Tanzania Bara yatajengewa vituo vya afya na tayari tuko hatua za mwisho za kutoa fedha kwa ajili ya kujenga vituo hivyo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hicho cha Makanda ni miongoni mwa vituo ambavyo vipo kwenye orodha hiyo na amefuatilia mara kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wawe na uhakika na hilo, lakini kuna majimbo 18 ambayo mpaka sasa hatujapata mapendekezo ya kata ambazo wanahitaji kujenga vituo vya afya. Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge ambao hawakuleta taarifa ya kata ambazo wanapendekeza, watuletee ili tukianza kutoa fedha kata hizo ziwe sehemu ya mradi huo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi, Kituo cha Afya cha Mpengele kwenye Kata ya Mkata, ni miongoni mwa vituo vya afya vya mwanzo kabisa, lakini hakina jengo la *OPD* mpaka leo. Je, Serikali iko tayari kutuletea fedha kwa ajili ya kujenga jengo la *OPD*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Kituo hicho cha Afya cha Mpengele katika Kata hiyo ya Makata, Jimbo la Liwale, Mheshimiwa Kuchauka amefuatilia mara kadhaa na kwa bahati njema Serikali tulishaainisha vituo vya afya vyote vyenye majengo pungufu. Baada ya ukamilishaji wa vituo vya afya vya kimkakati tunakwenda kuanza na awamu ya pili ya kukamilisha majengo katika vituo vyenye majengo pungufu na vituo vya afya ambavyo ni chakavu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili tutalipa kipaumbele, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, je, ni lini Serikali itajenga jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya cha Mafiga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasikia kituo cha afya?

**MWENYEKITI:** Rudia swali.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itajenga jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya cha Mafiga? Mheshimiwa Waziri, hili swali nimeuliza mara nyingi na tumeongea wote pamoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Unakifahamu hicho kituo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma amefuatilia na ameuliza mara kadhaa kuhusiana na jengo hilo katika Kituo cha Afya cha Mafiga katika Manispaa ya Morogoro. Nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali sikivu imeshaweka mpango kwa ajili ya kwenda kujenga jengo hilo katika kituo hiko cha afya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, je, ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya cha Mwika? Nimeuliza swali hili toka nije hapa Bungeni, ile Novemba mpaka leo nauliza tu, lakini hamna mtu anayejibu wala hakuna kichachofanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei nilishakaa naye mara kadhaa na tulishakubaliana kwamba Kituo cha Afya cha Mwika kiko kwenye mpango wa Vituo vya Afya vya Benki ya Dunia na nilimuonesha kwamba kipo kwenye orodha hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba ni suala la taratibu tu za kifedha na kituo kile tayari kitajengwa kupitia Mfuko wa Benki ya Dunia, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali upande wa afya, Kata ya Mlowa, Kijiji cha Mkolango, wananchi wamejenga zahanati kwa nguvu zao, Diwani pamoja na mimi Mbunge. Ni lini Serikali itaunga mkono jitihada za wananchi katika zahanati hiyo ya Mkolango?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ambaye ni Mwenyekiti wa Wabunge wote wa Mkoa wa Njombe, lakini pia ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi kwa Mkoa wa Njombe na Mbunge wa Jimbo la Makambako, amefutilia mara nyingi sana kuhusiana na Zahanati ya Mkolango na mimi nimeshamhakikishia kwamba tumeshaingiza kwenye mpango wa zahanati ambazo zitapelekewa shilingi milioni 50. Nimhakikishie tu kwamba mpango huo bado upo palepale na tutahakikisha kwamba tunautekeleza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Kata ya Mtunda ni moja katika kata za mkakati katika Jimbo la Kibiti ukizingatia kwamba kata hii ni moja ya kata ambazo zilikuwa zimekumbwa na mafuriko katika kipindi

kilichopita, je, nini kauli ya Serikali katika kuweza kujenga kituo cha afya kwa wananchi wale ambao wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kata zote za kimkakati ambazo halmashauri zilikubaliana na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeziwekea mpango wa utekelezaji wa aina mbili; mpango wa kwanza ni kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, lakini mpango wa pili ni kupitia fedha za Serikali Kuu. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mpembenwe kwamba amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na kituo hicho cha afya na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeweka kipaumbele kuhakikisha kwamba wananchi wa kata hiyo wanapata kituo cha afya ili waweze kupata huduma bora za afya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaipandisha hadhi Zahanati ya Buchambi, Wilaya ya Maswa, kwa vile inahudumia watu wengi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishaji wa hadhi wa zahanati kuwa kituo cha afya upo kwa mujibu wa utaratibu ambao halmashauri kwanza baada ya kufanya tathmini ya idadi ya wananchi walioko katika eneo hilo, ukubwa wa usiopungua ekari 15, lakini pia na umbali kutoka kituo cha jirani zaidi cha afya wanaweza kuwasilisha maombi ya kupandisha hadhi kituo hicho ili Serikali ianze kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga, kupanua na pia kuanza kutoa huduma ngazi ya kituo cha afya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na TAMISEMI, nimuite Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Nusrat Hanje.

Na. 90

**Kukamilisha Maboma ya Zahanati, Kyerwa**

**MHE. NUSRAT S. HANJE K.n.y. MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, maboma mangapi ya zahanati hayajakamilika Wilayani Kyerwa na lini yatakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ina jumla ya maboma ya zahanati 17. Katika mwaka 2022/2023 na 2023/2024 Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ilipokea shilingi milioni 200, kwa ajili ya kukamilisha maboma ya Zahanati za Kaina, Businde, Rwensheshe na Katera. Zahanati ya Katera imekamilika na inatoa huduma, Zahanati za Kaina, Businde na Rwensheshe ujenzi upo hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa imetenga shilingi milioni 140 kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa boma la Zahanati ya Rwanyango, nyumba za watumishi katika Zahanati ya Chanya na Iteera, pamoja na ujenzi wa jengo la kliniki katika Zahanati ya Rukuraijo. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati kote nchini yakiwemo maboma ya zahanati katika Halmashauri ya Kyerwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Wilaya ya Ikungi, Jimbo la Singida Mashariki, Kata ya Ntuntu, wananchi wamejiunga na wamejenga boma la Zahanati ya Mampando, pia kuna Kata nyingine ya Mungaa ambayo wananchi wamejiunga na wamejenga boma la Zahanati ya Kinku, lakini mpaka sasa hivi bado Serikali hawajamaliza.

Sasa niwaulize Serikali ni lini watapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma haya mawili ya zahanati upande wa Singida Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa nini Serikali isifanye tathmini nchi nzima kufahamu maboma ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi kwa sababu tunapenda wananchi washiriki katika maendeleo ili sasa kabla ya kwenda kwenye kujenga zahanati nyingine mpya waanze kukamilisha haya ambayo wananchi wamejiunga na wametumia nguvu zao kujenga maboma? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki kwa kuchangia nguvu zao na kujenga maboma hayo mawili ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Nimhakikishie tu kwamba katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo ya fedha Serikali imeendelea kupeleka fedha kila mwaka angalau shilingi milioni 100, 150 hadi 200 kila jimbo, kila halmashauri, kwa ajili ya ujenzi kwa ukamilishaji wa zahanati.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba maboma haya aliyoyasema nayo tutachukua taarifa zake tuone yameingizwa kwenye mpango upi ili yaweze kupelekewa fedha kwa ajili ya ukamilishaji, aidha kwa mapato ya ndani ya halmashauri au fedha kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali imeshafanya tathmini ya maboma yote kote nchini na tayari imeshaweka mpango wa utekelezaji na ndio maana kila mwaka wa fedha zaidi ya maboma 300 yanapelekewa fedha zaidi ya shilingi bilioni 15 tangu mwaka wa fedha 2021/2022 mpaka sasa na mwaka huu wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji. Mpango wa ukamilishaji unafuata ile orodha ya maboma ambayo yalitambuliwa. Nitumie nafasi hii kuwasisitiza Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kwamba lazima ujenzi huu wa maboma uratibiwe vizuri badala ya kujenga maboma kila siku na yanakaa muda mrefu kabla hayajakamilishwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, Zahanati za Kitelewasi na Rungemba ambazo zipo katika Jimbo la Mafinga zimejengwa kwa nguvu za wananchi. Nini mkakati wa Serikali kumalizia zahanati hizo ili ziweze kutumika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze wananchi wa Kitelewasi na Rungemba kwa kujenga maboma hayo ya zahanati kwa nguvu za wananchi. Nitumie nafasi kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mafinga kuhakikisha kwamba wanatenga fedha kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji, lakini pia wanaleta taarifa hizo Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuingizwa kwenye mpango wa maboma ya shilingi milioni 50, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tunaishukuru Serikali kupitia *TASAF* wametujengea zahanati katika Kata ya Bondeni, lakini mpaka sasa hivi zahanati ile imekamilika, hakuna vifaa tiba wala wataalamu. Je, ni lini

Serikali itatuletea vifaa tiba na wataalamu ili zahanati hii iweze kufanya kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Hai na Halmashauri ya Wilaya ya Hai ni moja ya halmashauri ambazo Mheshimiwa Rais amepeleka zaidi ya shilingi milioni 800 katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Hai, kwanza, kuhakikisha kwamba wana-*allocate* watumishi kwa ajili ya kuanza huduma za msingi kwenye zahanati hiyo, watumishi ambao wanapatikana ndani ya halmashauri.

Pili, wahakikishe kwamba wanapeleka vifaa tiba kwa sababu fedha tayari imeshapelekwa, ni suala la wao kufanya *redistribution* kuhakikisha kwamba vifaa hivyo vinapelekwa kwenye zahanati hiyo ianze kutoa huduma, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Mchakamchaka, Katobo, Isubangala, Mganza na Kapanga kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika wamejenga maboma ya zahanati yamefikia hatua ya lenta. Je, ni lini Serikali itaunga mkono jitihada za wananchi ili waweze kumalizia maboma hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, safari ni hatua, tumeshaanza kupeleka fedha katika Halmashauri ya Tanganyika kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa maboma ya zahanati. Niwapongeze wananchi wa vijiji hivyo vya

Mchakamchaka na vingine ambavyo wamechangia nguvu zao na kujenga maboma hayo, Serikali inatambua na kuthamini mchango wao na fedha itatafutwa kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, pia kupitia Serikali Kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea bado tuko TAMISEMI, nimuite sasa Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Sengerema aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Mabula.

Na. 91

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara za Sengerema Mjini**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA K.n.y. MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa kilometa 15 za barabara za Sengerema Mjini kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano ya ujenzi wa barabara kilometa 15 katika Mji wa Sengerema kwa kiwango cha lami ambapo hadi kufikia sasa kilometa 1.69 zilizogharimu shilingi milioni 974 zimekwishakamilika. Barabara zilizokamilika ni Kabita – Sengerema Sekondari kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 0.97 na CCM - Bwawani na Pambalu yenye urefu wa kilometa 0.72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Serikali inajenga barabara ya Mapinda – Lubeho Hotel kilometa 0.57 na Mabimbi - Beipoa kilometa 0.43 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi milioni 570 ambapo mchakato wa ununuzi unaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kufanya usanifu kwa

barabara zilizosalia zenye urefu wa kilometa 12.31 kwa lengo la kupata gharama halisi za ujenzi na pindi fedha inapopatikana ujenzi uanze mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niishukuru Serikali kwa majibu yake, naomba kuuliza kwamba ahadi ilikuwa ya kilometa 15 lakini mpaka leo miaka inakwisha ni kilometa 1.6 ndiyo imekamilika.

Je, ni lini hizo kilometa 12 zitakamilika kwa uhakika badala ya kwenda nusu nusu?

Swali la pili, tarehe 30 Januari, 2024 Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kilometa 12 katika Manispaa ya Ilemela, mpaka leo hakuna kilometa hata moja ambayo imeanza.

Je, ni lini kilometa hizo zitajengwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza maswali mazuri yenye lengo la kuboresha miundombinu ya barabara kwa ajili ya wananchi na hasa wale anaowawakilisha, lakini ambao Mheshimiwa Mbunge Tabasam anawawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza, ile ahadi iliyotolewa ya kilometa 15 ni ahadi ambayo tunaiweka katika kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa miradi hii ya ujenzi wa barabara. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa barabara hii haiwezi kujengwa kwa wakati mmoja kilometa zote ndiyo maana Serikali kila mwaka wa fedha inatenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga barabara hii kwa vipande. Kwa hiyo, nimhakikishie hata katika mwaka huu wa fedha, fedha zimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara inaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili ambayo ni ahadi katika Jimbo la Ilemela, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu ya barabara kwa maana ina maslahi makubwa kwa wananchi kiuchumi, lakini kijamii. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba Serikali itaendelea kutafuta fedha ipate fedha kwa ajili ya kujenga barabara hii.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa *Engineer* Tumaini Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ni lini Serikali itaanza uboreshaji wa miundombinu ya barabara za Mji Mdogo wa Katoro?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, hakika amekuwa akipambania maendeleo katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie kwamba Serikali kila mwaka wa bajeti inatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu ya barabara. Mathalani katika Serikali ya Awamu ya Sita, bajeti ya *TARURA* imeongezeka kutoka bilioni 275 mpaka kufikia bilioni 710.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hiyo ni dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba inafikia mtandao mkubwa zaidi wa barabara hizi kwa kuwa zina manufaa makubwa kwa wananchi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kila mwaka wa fedha itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha inazifikia barabara nyingi zaidi ikiwemo barabara katika Mji wa Katoro.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava. Waheshimiwa nimewaona wote.

**MHE. DKT. CHRISTINE C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayotoka Ndala kwenda Mwawaza, Manispaa ya Shinyanga ambako kuna Hospitali ya Rufaa, iko kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi lakini Makamu wa Rais alikuja Shinyanga akatoa ahadi.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii aliyoitaja iko kwenye mpango na fedha ikipatikana nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge dhamira ya Serikali ni kuhakikisha barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami ili iweze kuwanufaisha wananchi.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni lini barabara ya kutoka Vwawa – Londoni - Msiya hadi Isarawo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ambayo imekuwa ni ahadi ya muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha inafikia barabara nyingi iwezekanavyo, kupanua mtandao wa barabara hizi za Wilaya ziwe zina hadhi nzuri na ziweze kupitika katika kipindi cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kuhakikisha inatenga fedha kila mwaka na barabara hii ipo kwenye mpango, hivyo nimhakikishie kwamba barabara hii itajengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Ludewa kwenda Ibumi ilikuwa imefunga kutokana na mvua zilizozidi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ilituma wataalamu kuikagua hiyo pamoja na nyingine tatu na kuahidi zitapewa fedha kutoka *World Bank.*

Je, ni lini Serikali itatoa fedha hizo ili kabla ya mvua ziweze kufanyiwa matengenezo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, hakika amekuwa akizisemea sana hizi barabara kwa kuwa anatambua na ana matamanio wananchi wake waweze kupata barabara nzuri zenye hadhi nzuri ambazo zitawezesha shughuli za kiuchumi na kijamii katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizi kwa ajili ya dharura zimepatikana shilingi bilioni 170 na nimhakikishie kwamba hatua ambayo ipo sasa ni ya manunuzi, kupata wakandarasi ili waweze kuingia *site*. Nimhakikishie baada ya muda mfupi kutoka sasa tutawaona wakandarasi wako *site* kwa ajili ya kuanza kujenga barabara hizi.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais ya barabara ya *KCMC, YMCA* ambayo ina taasisi zaidi ya kumi na msongamano mkubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa tayari mimi na yeye tumeshazungumza kuhusiana na barabara hii na tayari tumeiweka katika vipaumbele kabisa iko kwenye mpango, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi fedha zitakapopatikana barabara hii inakuja kujengwa.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Mohamed Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, barabara ya kutoka Kwamtoro - Sanzawa - Mpendo yenye kilometa 54 imeharibika sana kwa sababu ya mvua kubwa iliyonyesha, hata hivyo, tumeleta maombi maalum.

Je, ni lini sasa Serikali italeta fedha ili tuweze kufanya ukarabati wa barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa maombi yake haya sisi tuliyapokea na tunayafanyia kazi ili tuweze kuhakikisha kwamba dhamira ya Rais inatimia ya kuhakikisha Watanzania wanapata barabara zilizo bora ambazo zinapitika katika misimu yote katika mwaka mzima.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunafanyia kazi maoni haya mahsusi kabisa na

pindi fedha zitakapopatikana tunakuja kuhakikisha kwamba tunajenga barabara hizi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Tabasam, lakini swali lako lilikuwa la msingi limeshaulizwa. Katika hali ya kawaida hutakiwi kuuliza, lakini nakupa tu nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba amesema katika kilometa 15 tunatengenezewa kilometa moja na nusu, sasa hiyo ni ahadi ya Rais wakati wa uchaguzi mwaka 2020.

Je, ni lini sasa TAMISEMI wataheshimu ahadi za Rais wanazozitoa katika kampeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya. Nilipata nafasi ya kutembelea Jimboni kwake na kwa kweli baadhi ya changamoto hizi aliziwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na yeye tayari tulishazungumza na nimemfahamisha kwamba suala lake hili la barabara na hasa hizi za ahadi ya Rais, ahadi za viongozi wakuu kwa kweli ni kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa majukumu yetu sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama tulivyozungumza, tunaweka msukumo kuhakikisha kwamba tunaendelea kujenga barabara hii kwa awamu kila mwaka tutakuwa tunatenga fedha ili mwisho wa siku ahadi ile iweze kutimia.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya halafu utafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi

ambavyo anatujibu kwa kujali maswali ya wananchi wa majimbo yetu, naomba niulize swali moja dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati amekuja Mheshimiwa Makamu wa Rais, Wilaya ya Nyasa, wananchi walikuwa wamempa kilio cha Daraja la Mto Likwilu ambalo lilibomolewa na maji miaka kama mitatu iliyopita, wale wananchi wanateseka sana na tumeandika maombi maalumu kuleta katika Wizara yako. Je, ni lini ombi hilo litatekelezwa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kumpa pongezi kubwa sana Mheshimiwa Mbunge, hakika mara kwa mara amekuwa akipaza sauti yake kwa ajili ya kuwaombea wananchi wake maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na maombi haya ni kweli yamepokelewa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi na yeye kwa pamoja tutaendelea kufuatilia ili mwisho wa siku tuweze kuhakikisha ahadi hii imetekelezwa kwa sababu ahadi za viongozi wakuu hakika ni kipaumbele katika utekelezaji na mipango tunayoweka kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba maombi yake tumeyapokea na kwa kweli tunayapa uzito unaotakiwa na nimhakikishie kwamba fedha zikipatikana kwa kweli Daraja la Likwilu litaenda kujengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwenye Kata ya Chiwale ulianza kwa kutumia fedha za Jimbo pamoja na fedha za tozo ambazo ziko *ring-fenced*. Hata hivyo, wakandarasi wengi wameji-*mobilize*

wameondoka maeneo yao ya kazi kwa sababu hawajapewa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kufahamu, ni kwa nini fedha hizi haziwafikii wakandarasi, nani anazishikilia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi yake nzuri anayoifanya ya uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili mahsusi kabisa naomba baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu mimi na yeye tuweze kukaa ili tuweze kufanya ufuatiliaji wa wakandarasi hawa ambao wame-*raise certificate* na bado hawajapata malipo yao, kwa sababu malengo ya kutaka wazawa waweze kushiriki katika zabuni kama hizi hasa za ujenzi wa miundombinu muhimu kama ya barabara, dhamira ni kuwawezesha wazawa. Kwa hiyo, hatuko tayari kuona kwamba wanaangamia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mimi na yeye tutafanya ufuatiliaji ili tuweze kupata muafaka wa wakandarasi hao.

**MWENYEKITI:** Ahsante, bado tunaendelea Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha barabara ya kutoka Buguma kwenda Mchigondo kimeliwa na maji. Sehemu hiyo imekuwa ni karaha kubwa sana kwa akina mama, watoto na wazee kupita. Nataka Mheshimiwa Waziri aniambie, ni lini tutaongozana naye aende pale, aone tu jinsi akina mama wanavyopita pale wakivuka? Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi wa wananchi wake. Kuhusiana na ombi lake mimi na yeye tutakaa tutajadili na tutapanga kwa ajili ya utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Bado tunaendelea Ofisi ya Rais, TAMISEMI nimwite sasa Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke, sasa aulize swali lake.

Na. 92

**Kujenga kwa Zege Barabara Zinazoingia Bandari Kavu-Temeke**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa zege barabara zinazoingia Bandari Kavu – Temeke?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Serikali kupitia Mradi wa *DMDP* Awamu ya Pili imepanga kutumia shilingi bilioni 1.8 kufanya ujenzi kwa kiwango cha zege barabara ya Markas kilometa 0.48 iliyoko Bandari Kavu Namba 20 na kujenga mfereji mkubwa wenye urefu wa kilometa 1.16 wa kutoa maji ya mvua ambayo yamekuwa yakisababisha mafuriko kwenye makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2024/2025, Serikali imepanga kujenga kwa kiwango cha zege barabara ya Saza kilometa 0.550 iliyoko Bandari Kavu ya Kontena Tupu, Fantuzz Chang'ombe kwa gharama ya shilingi milioni 750 na mkandarasi tayari yuko *site*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwa kuwa eneo la Kata ya Kurasini ndani ya Jimbo la Temeke ni eneo la uwekezaji. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga zile barabara za ndani ambazo kontena nyingi zinapita kwa kiwango cha zege?

Swali la pili, je, mko tayari kutengeneza barabara inayoitwa Kilima cha Nyani ndani ya Kata ya Vituka katika Jimbo la Temeke?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge. Mara kadhaa amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana kuhusiana na masuala ya miundombinu ya barabara katika Jimbo lake na mimi na yeye tumekuwa tukifanya kazi kwa ukaribu. Kwa hiyo, naomba niendelee kumhakikishia kwamba katika eneo hili la Kurasini ambalo ni eneo la uwekezaji, Serikali inaweka kipaumbele kikubwa sana na tayari ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha zege upo kwenye mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna fedha nyingi ambazo tayari zimepatikana kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam ikiwemo katika Jimbo lake, nimhakikishie tumeanza na maeneo mengine, lakini tutakuja kufika katika barabara hizi kwa umuhimu wake, kutokana na msingi mzima wa kuwa eneo la uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na barabara hii ya Kilima cha Nyani nimhakikishie kwamba barabara hii iko kwenye mpango na itajengwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimewaona Mheshimiwa Dkt. Pallangyo atafuatiwa na Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hii nafasi. Ninatumia pia nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuweza kujenga kwa kiwango cha zege

kipande cha barabara eneo Ndoombo ikiwa ni sehemu ya barabara ndani ya barabara inayoanzia Sangisi - Akheri hadi Ndoombo.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kuendelea na zoezi hilo la kujenga kwa zege barabara zote ambazo zinapanda milimani kule Meru, tukianza na eneo la Ulong'a - Kata Nkoanrua, eneo la Sela - Kata ya Seela Sing'isi, Sura - Kata ya Poli na Songoro - Kata ya Songoro? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, hakika mimi na yeye tumekuwa tukizungumza mara kwa mara kuhusiana na ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya barabara katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na barabara hizi za milimani ambazo kwa kweli amekuwa akizizungumzia mara nyingi sana hapa Bungeni, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumekwishaanza. Hii ni hatua ya kwanza na kila mwaka tutakuwa tunatenga fedha ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kuziboresha barabara hizi ili ziwe katika hadhi ya zege ambayo ina uimara zaidi na inayostahimili mazingira ya milimani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha zege Barabara ya Tinyango kuunganisha na Machimbo katika Kata ya Chamazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ya uwakilishi anayofanya na ya kuwasemea wananchi wake na hasa kwenye masuala ya miundombinu ya

barabara. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na barabara hii ya Tinyango anayoitaka ijengwe kwa kiwango cha zege kwamba barabara hii ipo kwenye mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka fedha zinatengwa kwa ajili ya kuendeleza barabara zetu hizi za wilaya na nimhakikishie kwamba ni kwa kadiri ya fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba inafikia barabara zote ikiwemo barabara hii aliyoitaja ya eneo la Tinyango**.** Kwa hiyo, tutalifikia Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Maretadu – Dongobesh – Haydom kwa kiwango cha zege kwa sababu barabara hii imekuwa ikichakaa kila mwaka na haipitiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya uwakilishi anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala lake la barabara zake kujengwa kwa kiwango cha zege hatua ya kwanza itakuwa ni kufanya usanifu na kubaini ni kiwango gani cha bajeti kinachohitajika kwa ajili ya kuziendeleza barabara hizi. Baada ya hatua hizo kukamilika, hatua zinazofuata zitachukuliwa ili hatimaye fedha ziweze kupatikana na kuhakikisha kwamba barabara zinaweza kuboreshwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza maswali ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ninawashukuru sana Naibu Mawaziri wote wawili wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujakwenda kwenye maswali yanayofuata au swali linalofuata niombe twende kwanza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuna mwenzetu kidogo ana

*emergence*. Kwa hiyo, nimwite sasa Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 104

**Muswada wa Sheria ya Sekta Binafsi ya Ulinzi Nchini**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza: -

Je, lini Muswada wa Sheria ya Sekta Binafsi ya Ulinzi utaletwa Bungeni kwa kuwa kampuni binafsi za ulinzi zilianzishwa bila sheria wala kanuni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Baran.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** ajliibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa sheria inayosimamia kampuni binafsi za ulinzi. Maoni ya wadau wa pande zote mbili za Muungano yamepokelewa na yanafanyiwa kazi kwa kina na mara yatakapokamilishwa muswada wa sheria utawasilishwa Bungeni, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali na kwamba ninaipongeza sana Serikali kwa kuwa na nia ya kuleta muswada huu hapa Bungeni, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Jeshi la Polisi limeanzisha Kampuni ya Ulinzi Binafsi, wakati huo huo Jeshi la Polisi ndio wasimamizi wa sekta hii ya ulinzi binafsi, kampuni za ulinzi zinaona kwamba suala la Jeshi la Polisi kuanzisha kampuni ya ulinzi litaleta ushindani mbaya kinyume na matakwa ya Tume ya Ushindani.

Je, Serikali inasema nini kuhusu suala hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Baran Sillo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya ulinzi iliyoanzishwa na aliyosema ya polisi si ya Jeshi la Polisi ni ya Shirika la Uzalishaji la Polisi, ni shirika ambalo linafanya biashara kama shirika lingine. Kwa hiyo, siyo kampuni ya Jeshi la Polisi *per-se,* ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Kwa vile kuna swali lingine la Wizara ya Mambo ya Ndani, nimwite sasa Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, naye aulize swali lake.

Na. 105

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Jimbo la Kilindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishatenga fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilindi kutoka kwenye bajeti ya Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kiasi cha fedha shilingi milioni 800 zitatumika katika kukamilisha ujenzi huo. Maandalizi ya ujenzi yanaendelea na kiasi cha fedha shilingi milioni 400 zimekwishakutolewa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kwanza kwa dhati ya moyo wangu na kwa niaba ya Wana-Kilindi ninaomba niipongeze Serikali kwa sababu lilikuwa

ni jambo la muda mrefu sana, sana, sana. Niombe tu kwamba Serikali au Wizara ya Mambo ya Ndani iharakishe kwa ajili ya kuanza ujenzi huo, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Kikunde wamejenga Kituo cha Polisi na kimefikia 99%. Kwa utaratibu ule ule wa ku-*support* nguvu za wananchi; je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutenga kiasi cha fedha ili kuwa-*support* wananchi wa Kata ya Kikunde?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunapokea pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo cha Polisi cha Kata alichokitaja Mheshimiwa Mbunge, ni kweli tunajenga na kwamba tunamalizia maboma ambayo tayari wananchi wamekwishaonesha juhudi zao za kujenga vituo hivyo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo chake hicho pia tutakichukua tukiongeze kwenye mpango ili tukimalizie na ili wananchi wapate huduma ya ulinzi na usalama katika eneo lao, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, nimekuona.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa kujenga au kukarabati kile Kituo cha Kegonga ambacho kilikuwa katika hali mbovu sana, sasa hivi kimekuwa cha kisasa. Sasa ninataka kujua, je, ni lini Serikali itajenga kituo cha polisi katika Kata ya Susuni ambayo haina kabisa kituo cha polisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapokea pongezi kwa kituo cha kisasa ambacho tayari kimekwishakamilika. Kuhusu Kituo cha Polisi cha Kata ya Susuni, tunajenga hivi vituo vya polisi awamu kwa awamu. Nimhakikishie Mheshimiwa Esther kwamba kituo chake cha Kata ya Susuni kitaingia kwenye mpango na tutakitengea fedha na kitajengwa, kwa sababu nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kila kata katika nchi hii inapata kituo cha polisi kwa ajili ya usalama wa raia na mali zao, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Baran Sillo tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, turudi kwenye *Order Paper* yetu, twende Wizara ya Nishati. Nimwite Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 93

**Fidia kwa Wananchi wa Nanyumbu, Kupisha Ujenzi wa Gridi ya Taifa**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu ili kupisha ujenzi wa Gridi ya Taifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Nanyumbu wananchi 689 wanapisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 kutoka Tunduru hadi Masasi. Taratibu za kuwalipa fidia wananchi waliopisha mradi zinaendelea ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.95 zinatarajiwa kulipwa kwa wananchi hao. Aidha, kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kulipa fidia wananchi hao ambapo fedha zitakapopatikana watalipwa stahiki zao kwa wakati, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa Gridi ya Taifa ni muhimu sana katika Jimbo langu la Nanyumbu na kwa Serikali kwa ujumla. Sisi tunaamini kabisa kwamba mradi huu ukimalizika ile katika katika ya umeme kwenye Jimbo la Nanyumbu itakwisha, lakini nina maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekwishaachia mashamba yao huu ni mwaka wa pili sasa na mashamba yale ya mikorosho ndicho kilichokuwa chanzo kikuu cha uchumi kwa wananchi wale. Sasa nataka nipate *commitment* ya Serikali: -

(a) Je, ni lini itawalipa wananchi wale fedha zao ili kufidia yale machungu ya kuyaacha maeneo yale?

(b) Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari hiyo *commitment* atakayoitoa akaja ndani ya jimbo langu akaongea na waathirika wa hili eneo ili wananchi wale waridhike kupata majibu moja kwa moja kutoka Serikalini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze, amekuwa akifuatilia juu ya fidia hii ya wananchi wa Nanyumbu kwa muda sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni mradi wa kimkakati ambao unalenga kupeleka umeme wa gridi kwenye Mikoa ya Mtwara na Lindi, kwa hiyo, ni mradi ambao kwa kweli ni kipaumbele kwa Serikali. Vivyo hivyo suala la fidia pia ni suala ambalo tunaliangalia kwa jicho la kipekee. Niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa wananchi wake wa Nanyumbu watalipwa fidia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wakati anafanya ziara katika Mkoa wa Mtwara aliwahakikishia wananchi wale kwamba watalipwa fidia. Mimi niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itawalipa fidia wananchi wake wa Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mimi kwenda kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge nitafika na tutaenda kwa wananchi pamoja na Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa changamoto ya ukosefu wa umeme wa Gridi ya Taifa, lakini pia mitambo mizuri ya umeme inawakumba wananchi wa Kigamboni katika Kata za Kigamboni, Vijibweni, Mji Mwema, Gezaulole, Somangira, Kibada, *Kisarawe II* na Mwasonga kukosa umeme wa uhakika kwamba ikifika saa 12.00 jioni kunakuwa na *low voltage* kiasi kwamba maeneo hayo huwezi kupika, huwezi kuwasha *microwave,* huwezi kuwasha chombo chochote na umeme unakuwa kama wa kibatari.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaondolea kero hiyo wananchi wa Kigamboni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni kweli kwa yale maeneo ya Kigamboni ikifika jioni umeme unakuwa na *low voltage*. Serikali tayari imekwishaanza kulifanyia kazi jambo hilo. Kupitia Kituo cha Kupooza Umeme cha Mbagala tumeongeza transfoma nyingine ili kuhakikisha kwamba tunaongeza nguvu ya umeme kwa ukanda wote ule kuanzia Kigamboni, Mbagala mpaka kwenda Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, transfoma ile imekwishafika na mkandarasi yuko *site*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inafanya kila jitihada ili

kuhakikisha kwamba wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam hususan maeneo ya Mbagala, Kigamboni na Pwani wanaendelea kupata umeme wa uhakika na hivi karibuni mradi utakamilika na umeme utakuwa wa uhakika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa, ahaa, kuna swali lingine. Basi nimwite Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 94

**Kupeleka Umeme Vitongoji Visivyokuwa na Umeme – Bukoba Vijijini**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme vitongoji visivyokuwa na umeme Bukoba Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuunganisha vitongoji ambavyo havina umeme ambapo vitongoji 258 kati ya 515 vya Jimbo la Bukoba Vijijjini vimefikishiwa umeme. Aidha, kazi ya kupeleka umeme katika vitongoji 27 ambavyo havina umeme katika Jimbo la Bukoba Vijijini inaendelea kupitia Miradi ya Ujazilizi 2B na mradi wa kupeleka umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili A *(HEP IIA)*. Serikali itaendelea kupeleka umeme katika vitongoji vya Jimbo la Bukoba Vijijini kupitia miradi inayotarajiwa kufanyika mbeleni, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na nipende kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa sana na nzuri inayoifanya katika kupeleka

umeme Jimbo la Bukoba Vijijini. Pamoja na hayo nina maswali mawili madogo ya nyogeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Jimbo la Bukoba Vijijini ni kubwa sana, lina vijiji 94 na vitongoji kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri vitongoji 515 na vitongoji ambavyo vimepewa umeme ni nusu ya vitongoji vilivyopo.

Je, hawaoni kwamba ni vyema katika mgao ujao Bukoba ipewe kipaumbele badala ya vitongoji 15 vipewe 60 au 100 kusudi watu wapate umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunafahamu kwamba kufunga umeme vijijini ni shilingi 27,000 kwa nyumba, lakini watu wangu wanaombwa 300,000/400,000 badala ya shilingi 27,000 na ni vijijini, je, ni kwa nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kuhusiana na kupeleka umeme kwenye vitongoji ambavyo bado havina umeme, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari kuna miradi inaendelea katika Jimbo la Bukoba Vijijini na tunatarajia kuwa na mradi mkubwa wa kupeleka umeme pia kwenye vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya yanatofautiana, na ni kweli kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge takribani nusu ya vitongoji havina umeme. Tutaendelea kushirikiana na Taasisi yetu ya Wakala wa Nishati Vijijini kuhakikisha kwamba maeneo ambayo kwa kweli miradi ya vitongoji ipo nyuma yanapewa jicho la kipekee ili kuhakikisha kwamba nayo yanapanda kidogo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, miradi ipo ambayo inafanyika, lakini na kwa miradi inayokuja tutaendelea kuhakikisha Bukoba Vijijini tunaingalia kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la pili la maeneo ya vijiji ambayo yanakuwa-*charged* shilingi 321,000. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na ni kweli kwenye baadhi ya maeneo yake ambayo ni vijiji kuna baadhi ya eneo kama moja au mawili

yanakuwa-*charged* shilingi 321,000. Kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati nimwelekeze Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO* kuyapitia maeneo haya ambayo ni vijiji na kwa namna moja ama nyingine yanakuwa-*charged* zaidi ya bei ambayo Serikali imetoa mwongozo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anton Mwantona, nilikuona.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua ni lini Mradi wa *REA* kwa vitongoji 15 katika Jimbo la Rungwe utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante mradi wa vitongoji 15 katika Jimbo la Rungwe, mkandarasi yuko *site* na sasa hivi anafanya manunuzi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mradi umeanza na tumeshasaini mkataba na huu mradi wa vitongoji 15 utaenda kutekelezeka, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Selemani Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji imeanza hata Jimboni kwangu Bukene Kampuni ya *Sinotech* imefika na imeanza kazi hiyo. Hata hivyo wanapeleka umeme kwenye vitongoji ambavyo tu vimepitiwa na *line* kubwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hata vile vitongoji ambavyo havipitiwi na *line* kubwa *(high tension)* navyo vinapata umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba huu mradi wa vitongoji 15 ni mradi jazilizi, kwa hiyo unatekelezwa kwenye maeneo ambayo tayari yana miundombinu. Kwa maeneo ambayo hayana miundombinu tunakuja na mradi kuanzia mwezi wa 12 ambao utahusisha kujenga *MV* na *LV lines,* lakini vilevile utahusisha kuweka transfoma

kulingana na ukubwa wa maeneo tofauti tofauti. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba yale maeneo ambayo hayana miundombinu na kwa hiyo, yameshindwa kunufaika na huu mradi wa ujazilizi wa vitongoji 15 yataendelea kupata umeme na yataendelea kujengewa miundombinu kwa mradi unaokuja wa kupeleka umeme kwenye vitongoji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Minza Mjika.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji vya Mkoa wa Simiyu ambavyo bado havijapata umeme ili kuondoa kero kwa wananchi wa Mkoa wa Simiyu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa kupeleka umeme kwenye vitongoji katika Mkoa wa Simiyu na sasa hivi tuna huu mradi wa ujazilizi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 15 katika majimbo yote ya Mkoa wa Simiyu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mkoa wa Simiyu ya kwamba Serikali itaendelea kupeleka miradi kwa kadiri tunavyoendelea mbeleni, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Francis Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa vitongoji ambavyo vinapitiwa na umeme mkubwa bado viko vingi sana kwenye majimbo yetu.

Je, Serikali haioni kuwa kuna sababu ya kuwaongeza hawa wakandarasi ambao wako *site* vitongoji zaidi ili kuokoa muda na kwamba tayari miundombinu ipo kwenye baadhi ya vitongoji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ni hatua na Tanzania nzima tuna vitongoji zaidi 36 ambavyo havina umeme. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vitongoji vyote vinapelekewa umeme. Hata hivyo ni mradi ambao ni lazima uende kwa awamu kwa sababu vitongoji hivi ni vingi. Tumekwishaanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge waendelee kutuvumilia, tunatafuta fedha mwezi wa 12 tunakuja na mradi mwingine na vitongoji vingi zaidi vitanufaika na miradi hii ambayo kiukweli ina tija kubwa sana kwa maeneo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wetu wa Tanzania, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri Judith Kapinga ninakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nimwite sasa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, aulize sawali lake.

Na. 95

**Wanafunzi Waliorudi Shuleni Baada ya Kujifungua**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza: -

Je, wanafunzi wangapi wamerudi shuleni baada ya kujifungua, tangu Serikali iruhusu wanafunzi hao kuendelea na masomo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kipanga.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa Waraka wa Elimu Na. 2 wa mwaka 2021 kuhusu urejeshwaji shuleni wanafunzi waliokatiza masomo katika elimu ya msingi na sekondari kwa sababu mbalimbali na mwongozo wa kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatiza masomo katika elimu ya msingi na sekondari kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya wanafunzi waliojiunga tena na shule baada ya kukatiza masomo walikuwa 22,844 ambapo kupitia mfumo rasmi ni 5,142 na mfumo usio rasmi ni 17,702.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa elimu kwa wanafunzi wa kike, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaendelea kusimamia utekelezaji wa Waraka tajwa, ili kuhakikisha kuwa wanafunzi waliopata ujauzito wanarejea shuleni na kutimiza ndoto zao za kielimu, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti kidogo. Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana Serikali kwa majibu. Idadi ya wanafunzi 22,844 ni idadi kubwa sana, je, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba idadi hii inapungua, ili wanafunzi wasipate ujauzito tena? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, wanafunzi wanaonyonyesha utaratibu wao upoje wanapokuwa wanaendelea na masomo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anataka kufahamu mikakati ya Serikali na ninaomba nimhakikishie na nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeweka mikakati mbalimbali ili kupunguza au kuondoa kabisa hii changamoto ya watoto wetu kupata ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la kwanza ambalo tunalolifanya kwenye maeneo ambayo tumeona yana changamoto kubwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na miundombinu ya mabweni pamoja na *hostel* kwa ajili ya vijana

wetu watoto wa kike ili kuondoa ile changamoto ya kwenda na kurudi shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, tumehakikisha kwamba katika kila taasisi yetu ya elimu, kuanzia shule zetu za msingi, sekondari mpaka vyuo vikuu tunakuwa na madawati maalumu ambayo yanatoa ushauri pamoja na unasihi wa vijana wetu juu ya makuzi yao na mabadiliko ya kimwili kwa ujumla na kuhakikisha kwamba wanakwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, tumeanzisha somo maalumu la maadili katika shule zetu zote na somo hili linaanza kufundishwa kupitia mtaala wetu huu mpya na sera yetu mpya ya elimu. Vilevile tunahakikisha kama Serikali tunasimamia sheria, kanuni na taratibu kuhakikisha wale wote ambao wanafanya vitendo vya unyanyasaji kwa vijana wetu wanachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili kuhusiana na utekelezaji wa waraka huu kwa wale wanafunzi ambao wanaorudi shuleni, ni namna gani hatuathiri makuzi ya mtoto aliyezaliwa na vilevile hatuathiri taaluma ya mwanafunzi ambaye ameendelea na masomo. Katika maeneo yote ambayo wanarudi, waraka wenyewe umetoa mwongozo wa namna gani ya kumu-*handle* au kuhakikisha kwamba tunamlea yule mtoto katika mazingira mazuri. Pia kwenye maeneo yale vituo vyetu tumeanzisha vyumba maalumu kwa ajili ya kulelea wale watoto wakati akinamama wapo madarasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia posho japo kidogo kwa wanafunzi hawa ili kuhakikisha wanabaki shuleni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Maryam Mwinyi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maryam anashauri kwamba tuangalie namna gani ya kuweza kutoa posho kidogo. Hatuwezi kusema moja kwa moja jambo hili utekelezaji wake unakuwaje na kwa namna gani katika miongozo ya Serikali, lakini tubebe kama ushauri na twende tukaufanyie *evaluation* au tathmini tuweze kuangalia kama namna gani tunaweza kutekeleza au laa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munira, swali la nyongeza.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha wanafunzi hawa wanaorudi shuleni kwa mpango huu, wanaweza kumaliza masomo yao na kutimiza ndoto zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Sijasikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munira, hebu rudia swali lako alipate vizuri.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha wanafunzi hawa wanaorudia masomo yao kwa mpango huu, wanamaliza masomo yao na kutimiza ndoto zao?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la nyongeza kwenye mikakati mbalimbali ya Serikali, siyo tu kwa hawa ambao wanarudi hata kwa wale ambao wanaendelea na masomo, mikakati ni kama vile nilivyokwishaeleza awali kuhakikisha kwamba tunatengeneza mabweni, vilevile kutengeneza sheria zetu vizuri, kutoa elimu ile ya

unasihi pamoja na nasaha mbalimbali ili kuhakikisha hawa sasa hawaingii tena kwenye changamoto hii ambayo ilikuwa imewapata hapo awali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali kwa ujumla wakawa tayari kuleta takwimu za wanafunzi walioolewa, waliopata mimba ili tujue ukubwa wa tatizo tujaribu kutafuta mipango mizuri ya kuzuia shida hii? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Waitara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zipo na kama nilivyoeleza hapo mwanzoni kwamba mpaka kufika Machi, 2024 zaidi ya wanafunzi 22,000 waliweza kurejea shuleni kwa wale ambao walipata ujauzito kwa namna moja au nyingne. Hata hivyo, Mheshimiwa Waitara wewe unafahamu umeshawahi kuhudumu kwenye Serikali. Tuna takwimu zile ambazo tunazichukua za kila mwaka katika shule zetu zote. Kwa hiyo, tuna takwimu ya kila mwanafunzi mahali alipo na kama amekatiza masomo kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, tupo tayari kuziwasilisha takwimu hizo kwa kadiri zitakavyohitajika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyoneza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi, mimi nipo kwenye hiyo Kamati ya Elimu na kwa sababu tumeona kuna changamoto ya wazazi na walezi kutoa ushirikiano kwa watoto hawa ambao wanarudi shuleni baada ya Serikali kusema warudi shuleni.

Sasa Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba wazazi na walezi wanapewa elimu ya kutosha ili washirikiane na hawa watoto ambao wanarudishwa shuleni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na nimshukuru sana Mheshimiwa Nusrat Hanje nikijibu swali lake dogo na kwa vile yupo kwenye Kamati yetu ya Elimu, Utamaduni na Michezo na waraka huu unaeleza vizuri namna gani wazazi na walezi watashirikishwa kwenye malezi na makuzi ya watoto wetu ambao wanarejea shuleni. Kwa misingi hiyo, tuna Kamati Maalum katika kila shule za kuhakikisha kwamba wale watoto ambao wanarudi, Kamati ile iweze kushirikiana na wazazi na walezi kuhakikisha kwamba mtoto wetu anabaki salama, vilevile na makuzi ya mtoto aliyezaliwa yanakwenda katika hali ya usalama. Kwa hiyo, waraka wetu upo vizuri na unaelekeza mambo yote kwa ufasaha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kwenye Wizara hiyo hiyo. Nimwite sasa Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, sasa aulize swali lake.

Na.96

**Elimu ya Uzalendo kwa Wananchi**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ya uzalendo kwa wananchi wakati Taifa lipo katika mageuzi makubwa ya uchumi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Serikali imekuwa ikitoa elimu ya uzalendo kwa wananchi kupitia majukwaa mbalimbali kama vile vyombo vya habari na matamasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kutoa elimu ya uzalendo kwa kizazi cha sasa na baadaye, ilifanya maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya

mwaka 2014 pamoja na Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu wa mwaka 2023 ambapo katika maboresho hayo elimu ya uzalendo imetiliwa mkazo na itakuwa ikifundishwa katika Somo la Historia ya Tanzania na Maadili kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita. Somo hili litabeba maudhui yanayolenga kumjenga Mtanzania kuwa mzalendo na mwajibikaji anayefahamu historia, desturi, mila na maadili ya nchi yake.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali moja, kwa kuwa somo hili linatakiwa kufundishwa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu tu. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kufundisha somo hili la uzalendo katika vyuo vya kati na vikuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa sera tayari imekubalika ya mtaala huu, je, sasa Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri inaweza ikatuhakikishia kuwa ni lini litaanza kusomeshwa katika shule kwa mustakabali wa vijana wetu na nchi yetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pondeza, Mbunge wa Chumbuni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uboreshaji wa mitaala yetu ni suala ambalo ni *dynamic* siyo *static*. Ni mitaala ambayo inatakiwa iboreshwe kila wakati kulingana na mahitaji ya wakati huo. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kuwa Serikali kupitia vyuo vyetu hivi alivyovitaja vya kati na elimu ya juu tunaendelea kufanya maboresho ya mitaala yetu yote ili kuhakikisha kwamba somo hili la uzalendo

linakuwa ni sehemu ya masomo yatakayofundishwa katika vyuo vyetu vya kati na juu.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ushauri wake tumeupokea na wakati wa maboresho ya mitaala yetu katika vyuo vyetu vya kati utazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili anauliza juu ya lini mtaala huu mpya na sera yetu mpya imeanza kutekelezwa. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kuwa mtaala huu tayari tumeanza kuutekeleza kutoka mwezi Januari 2024, lakini tunatekeleza kwa awamu. Kwa hiyo, kwa awamu ya kwanza tunatekeleza kuanzia elimu ya awali, darasa la kwanza na darasa na la tatu. Vilevile kwa upande wa sekondari tumeanza kutekeleza mtaala mpya ambao unabeba masomo haya kwa kidato cha kwanza mwaka huu na kwa ule mkondo wa amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vyuo vya ualimu vilevile umeanza mwaka huu. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mtaala huu tayari Serikali imeshaanza kuufanyia kazi na utekelezaji wake umeanza toka mwezi Januari, 2024. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninakushukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nauliza, Wizara ina mkakati gani kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhakikisha vijana wetu wa Kitanzania wanapata elimu ya uzalendo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba elimu hii ya uzalendo tumekuwa

tukiitoa kupitia makongamano pamoja na mitandao na vyombo vyetu vya habari. Pia nimezungumza kwa suala la ushirikiano Serikali tunafanya kazi kwa dhana ile ya *collective responsibility,* kwa maana Wizara moja inapokuwa na jambo kwenye Wizara nyingine lazima tuweze kushikiriana kuhakikisha kwamba tunatekeleza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe wasiwasi kwa vile sasa masuala haya ya uzalendo na maadili yatakuwa yanafundishwa katika shule zetu kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vikuu, bila shaka huko tunapokwenda ni kuzuri na kwa maana hiyo vijana hawa watakapotoka watakwenda kuhudumu kwenye maeneo mengine, katika Wizara nyingine ambayo bila shaka elimu hii watakuwa nayo toka wakiwa wadogo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hali ya sasa ilivyo uzalendo kwa wananchi tulio wengi ni changamoto na Serikali imesema kwamba imekuwa ikitoa elimu hii kwa wananchi. Je, haioni sasa ni wakati wa kuongeza juhudi kuhakikisha elimu hii inawapata watu wote kwa ufasaha na kuweza kuwa chachu kwa kuelimika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli jambo hili ni muhimu kwa wananchi wote, lakini nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, yeye ni Mbunge na vilevile ni Diwani kwenye halmashauri au jimbo lake, mambo haya yamekuwa ni ajenda muhimu hata katika Mabaraza yetu ya Madiwani. Kwa hiyo, tunachukua ushauri wake, vilevile tuweze kuhakikisha na sisi kama Wabunge kwenye Mabaraza yetu ya Madiwani kwamba elimu hii inawafikia Madiwani na wananchi wote katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Omari Kipanga kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Kilimo, nimwite sasa Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 97

**Mkakati wa Kupandisha Kiwango cha Mauzo ya Kahawa**

**MHE. NEEEMA G. MWANDABILA** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kupandisha kiwango cha mauzo ya kahawa kitakacholipwa benki badala ya shilingi milioni moja inayolipwa kwa sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali iliweka utaratibu wa wakulima wanaouza kahawa kulipwa fedha za mauzo ya kahawa zaidi ya shilingi milioni moja kupitia akaunti zao za benki kwa madhumuni yafuatayo:-

(i) Kuondoa hatari za wakulima kuibiwa fedha zao za mauzo ya kahawa na kuhakikisha wakulima wanapokea fedha za mauzo kwa uharaka na usalama;

(ii) Kudhibiti upotevu wa fedha za wakulima kupitia vyama vya ushirika;

(iii) Kuongeza jitihada za kuwajumuisha wakulima wa kahawa kwenye mifumo rasmi ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali haina mpango wa kupandisha kiwango kinacholipwa kupitia benki kwa sababu kiwango hiki bado ni kikubwa na kinakidhi mahitaji ya lazima kwa wakulima. Kuongeza kiwango hiki ni kuongeza hatari za kiusalama na kufifisha azma ya Serikali ya kutumia mifumo ya kidjiti katika ulipaji wa fedha nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza. Awali ya yote kwanza niwapongeze kwa sababu zao la kahawa kipindi hiki lipo juu sana kwa bei yake sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa zao la kahawa limeonekana ni fursa ya kiuchumi, je, wana mkakati gani wa kuongeza idadi kubwa ya wanawake watakaoshiriki katika hiki kilimo cha kahawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa benki ya *KCBL* imekuwa Benki ya Taifa ya Ushirika, je, benki hii ina mkakati gani wa kupeleka huduma katika vituo vya kuuzia kahawa Mkoani Songwe? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya mkakati wa Wizara ya Kilimo ni kuhakikisha wanawake wanajihusisha na kilimo cha kahawa kwa kiwango kikubwa na huo ndiyo mkakati ambao tupo nao na ndio maana kati ya mashamba ya mfano kwa maana ya *block farms,* tumekuwa tukiwa-*engage* wanawake. Moja ya mfano wa shamba zuri lipo kule Mkoani Kagera katika Wilaya ya Muleba ambapo vijana na akinamama wamehusishwa kwenye kilimo cha kahawa. Kwa hiyo, ni sehemu ya mkakati wetu na tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Ushirika ambayo tumeizindua hivi karibuni ni kwamba kwa sasa itakuwa na matawi

makubwa matatu kwa maana ya katika eneo la Dodoma itakuwa ndiyo makao makuu, Kilimanjaro pamoja na Tandahimba ambako ndipo ilipoanzia. Baada ya hapo tumekubaliana kwamba watafungua matawi ikiwemo katika Mkoa wa Songwe. Kwa hiyo, hili lipo katika mpango mkakati wa benki hiyo ambayo sisi kama Wizara tunaisimamia, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa David Silinde tunakushukuru kwa majibu yako.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, nimwite sasa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, aweze kuuliza swali lake.

Na. 98

**Kuongeza Thamani ya Zawadi Tamasha la Utamaduni**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa kuongeza thamani ya zawadi kutoka shilingi 150,000 hadi milioni kumi kwenye Tamasha la Utamaduni nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Hamis Mwinjuma.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tamasha la Utamaduni nchini ni tamasha ambalo limekuwa likisherehekewa na makabila mbalimbali kila moja kwa wakati wake hasa nyakati baada ya mavuno. Matamasha haya hayakuwa na zawadi maalumu zaidi ya kuwa na sherehe kubwa ya kiutamaduni ambayo inakutanisha watu wa kabila moja kula, kunywa na kusherehekea mafanikio ya mavuno yao mfano ikiwa ni Tamasha la Wasukuma la Bulabo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais iliona ni vema kuyaunganisha makabila hayo na kuwa na tamasha moja la kitaifa. Uratibu wa tamasha hili umekuwa ukifanyika na Wizara yetu kwa kushirikiana na Ofisi ya

Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mkoa mwenyeji wa tamasha kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mkubwa uliofanyika tangu kuanzishwa kwake ni maboresho ya zawadi ambapo kwa tamasha la mwaka 2024 zawadi za fedha zilitolewa kwa vikundi, washindi wa kwanza katika mashindano ya ngoma za asili na uandaaji wa vyakula vya asili ilikuwa ni fedha taslimu shilingi milioni moja, kutoka katika shilingi 150,000 zilizotolewa mwaka kabla ya huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati uliopo hadi sasa pamoja na ukuaji mzuri wa tamasha hili, Wizara inaendelea na maandalizi ya kuwashirikisha wadau wa sekta binafsi ili kupata ufadhili zaidi na kuboresha zawadi ya tamasha lijalo ili tuendelee kulikuza Tamasha la Utamaduni wa Taifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza ninachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuona haja ya kuongeza zawadi hii kutoka shilingi laki moja hadi shilingi milioni moja kwa sasa. Niseme wazi kwamba mbali ya hizi zawadi Serikali imefanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Wizara kwa maandalizi ya tamasha la ugawaji wa tuzo, kwa maana ya *Tanzania Music Awards,* mmefanya kazi nzuri sana, tunawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa hili tamasha la utamaduni ambalo amekuwa akifanya kila mwaka nchi nzima, limekuwa linaleta tija na kulinda maslahi ya tamaduni zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninatoa rai kwa Serikali, ipi ni kauli yenu kwa matamasha haya kufanyika kwenye kila wilaya na kwenye kila mkoa ili kuhakikisha kwamba tunalinda utamaduni

wa nchi yetu hususani kwenye maeneo mbalimbali ya Taifa, ambapo utamaduni umekuwa ukipungua? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimetangulia kusema wakati ninajibu swali la msingi, matamasha haya yamekuwa yakifanyika katika maeneo mbalimbali, japo siyo kwa urasmi huu ambao umebebwa baada ya Serikali kuingilia kati na kulifanya tamasha la pamoja la utamaduni kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii sasa kuwaagiza Maafisa Utamaduni wa Wilaya na Mikoa, kwanza kuhakikisha wanashiriki na kuhakikisha matamasha ambayo yanafanyika katika maeneo yao yanafanikiwa na kama kuna mahali watakuwa wamekwama, sisi kama Serikali tuko tayari kushirikiana nao ili kuhakikisha matamasha haya ya utamaduni yanafana nchi nzima kutoka kabila moja hadi linguine, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Mheshimiwa Mbunge.

Tunakwenda Wizara ya Fedha, ninamwita sasa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 99

**Kupunguza Kodi ya Uingizaji wa Vyakula vya Samaki Nchini**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza kodi ya uingizaji wa vyakula vya samaki nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vinavyoagizwa kutoka nje na watu wanaojihusisha na ufugaji wa samaki na kilimo ambavyo Kamishna ameridhika kuwa ni kwa matumizi katika sekta ya ufugaji wa samaki, vimeondolewa Ushuru wa Forodha kwa mujibu wa kifungu cha 15(a) cha Sehemu B ya Jedwali la Tano ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani imetoa msamaha wa *VAT* kwenye uingizwaji wa vyakula vya mifugo ikiwemo vyakula vya samaki vinavyotambulika kwa *HS Code 23.09*, chini ya utaratibu wa utozaji ushuru wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini ninapenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itajipanga kuhakikisha vikundi vya wanawake na vijana katika Mkoa wa Ruvuma vinawezeshwa ili kuweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa chakula cha mifugo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka ruzuku katika chakula cha mifugo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Jacqueline kwa ufuatiliaji wa vikundi vya kinamama na ndiyo maana kila wakati huwa wanamchagua na tunamwombea uchaguzi ujao wamchague tena kwa sababu anawawakilisha vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imerejesha zile fedha kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya kinamama, vijana pamoja na makundi maalumu, kwa utaratibu mpya na uratibu wa vikundi hivi ili viweze kupata mikopo na kuweza kufanya shughuli za usindikaji vitaendelea kuratibiwa na ndani ya Serikali ni moja ya jambo ambalo tunalifanya na tena linafanyika kwa kuzingatia shughuli zinazofanyika katika kanda mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika ukanda ule vikundi hivyo vya usindikaji vitafanyika na maeneo mengine kufuatana na mazao yanayozalishwa katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ruzuku ya vyakula vya mifugo, tunaendelea kuongea na *sectors* ili kuweza kuona maeneo ambayo yanastahili kupata ruzuku. Tayari tunafanya katika baadhi ya maeneo ambako Serikali inatoa ruzuku. Kwa hiyo, tutaendelea kutoa ruzuku katika *sectors* mbalimbali kwa kuzingatia upatikanaji wa bajeti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mahawanga. Nilikuona Mheshimiwa Yustina Rahhi kwanza, halafu utafuatia Mheshimiwa Mahawanga.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza, nini mpango gani wa Serikali kupunguza kodi kama siyo kutoa ruzuku kwa viwanda vyetu vya ndani vinavyotengeneza vyakula vya mifugo, kuliko kuingiza vyakula vya mifugo kutoka nje? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametoa wazo zuri, Serikali tunalipokea na kwa kuwa tayari tunaenda kwenye utaratibu wa kuandaa bajeti mpya ya mwaka 2025/2026 kwenye hatua za kikodi haya ni mawazo mazuri ambayo tutayaweka kwenye kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tumekuwa tukifanya sana hiyo kwenye sera yetu ya *Import Substitution*, kutoa unafuu ama vivutio kwa wazalishaji wa ndani wa kila kitu kinachozalishwa ndani ili tuweze kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje kwa zile bidhaa ambazo tunaweza tukazizalisha kikamilifu ndani ya nchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni kwa namna gani Serikali inaweza kusaidia uzalishaji wa chakula nchini badala ya kutegemea uagizaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema katika swali lililotangulia, Serikali tunaweka vivutio kwenye uzalishaji wa bidhaa hizo kwa wazalishaji wa ndani lengo likiwa ni kujitosheleza ndani ya nchi ili kuweza kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ambao kiuchumi una madhara tunapokuwa na uagizaji mwingi kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo tutakapokaa na Kamati yetu ya Bajeti tutaendelea kupitia *item by item* ili kuweza kuhakikisha kwamba tunakuwa na maeneo mengi ambayo uzalishaji wake unafanyika ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameuliza maswali ya msingi, anaupiga mwingi kama ile timu ambayo hata ikifungwa haitumi wazee kufanya *press*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Wizara ya Afya, nimwite sasa Mheshimiwa Sylivia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 100

**Ongezeko la Wagonjwa wa Figo**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA K.n.y. MHE. SYLVIA F. SIGULA** aluliza: -

Je, nini chanzo cha ongezeko la wagonjwa wa figo nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la magonjwa ya figo hapa nchini kwa sasa yanachangiwa zaidi na sababu zifuatazo: -

(i) Ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza hususani shinikizo la damu pamoja na kisukari;

(ii) Matumizi holela ya dawa hasa zile za maumivu;

(iii) WAVIU wasiokuwa na ufuasi mzuri wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI;

(iv) Kutozingatia mtindo wa maisha unaofaa hususani matumizi makubwa ya chumvi, tabia bwete na matumizi ya vilevi hasa pombe na tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuielimisha na kuiasa jamii kuhusu kujikinga kwa kubadili mtindo wa maisha ambao unajumuisha ulaji usiofaa hususani matumizi makubwa ya chumvi, vyakula vyenye sukari nyingi au nafaka zilizokobolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeimarisha huduma za matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza pamoja na matibabu ya UKIMWI ili kuzuia madhara haya yasijitokeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja kwa niaba, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali.

Swali langu la kwanza, ni nini mpango wa Serikali kudhibiti matumizi holela ya dawa za binadamu ambayo imeonekana ni moja ya sababu inayochangia ugonjwa huu wa figo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ni nini mpango wa Serikali kuwezesha hospitali zake kutoa huduma ya kusafisha figo ili kuondoa adha wanayopata wagonjwa wa figo katika huduma na gharama za matibabu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Kainja kwa namna ambavyo anafuatilia masuala ya afya, hasa kwenye Mkoa wa Tabora ambao wakati wote amekuwa akifuatilia hata masuala ya watu binafsi kuhakikisha mambo yanakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, ni nini Serikali inafanya kuondoa matumizi holela ya dawa? Moja ni kuendelea kuelimishana na kutumia fursa hii kwamba matumizi ya dawa yazingatie maelezo ya daktari na unapokwenda kwenye duka la dawa, basi uwe umepata *prescription* ya daktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Waheshimiwa Wabunge mliona kampeni yetu na tumeleta katuni hapa inayozungumzia holela holela itakuletea matatizo. Maana yake tunaendelea na hilo suala la kuelimisha kuhusu alichosema dada yangu Mheshimiwa Kainja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, tunafanyaje kuhusu kuhakikisha tunawapunguzia wananchi mzigo wa matibabu hasa wanapopata matatizo wanapokwenda hospitali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, suala la Bima ya Afya kwa Wote na mmeona wiki hii Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa Arusha akiwa kwenye tamasha kubwa sana la kujipanga kuhakikisha tunafikia suala la Bima ya Afya kwa Watu Wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapambana kuhakikisha sasa vifaatiba, dawa na kila kitu tunakwenda kununua kiwandani moja kwa moja, badala ya kununua kwa wauzaji wa kawaida ili kushusha gharama ya matibabu kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ina utaratibu na ndiyo maana kila hospitali ina Maafisa Ustawi wa Jamii ambapo wale watu wanaoshindwa kulipa, basi kuna utaratibu wa kufuata ili waweze kutibiwa bila malipo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza, Aah, Mheshimiwa Paresso. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kusafisha figo kwenye Hospitali Binafsi na Hospitali za Serikali ina utofauti mkubwa wa bei. Hospitali Binafsi zina unafuu ukilinganisha na Hospitali za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ni kwamba ukienda kusafisha figo kwenye Hospitali za Serikali ni ghali zaidi kuliko Hospitali Binafsi; ni nini kauli ya Serikali kupunguza zaidi gharama hizi ili waathirika wa jambo hili waweze kupata unafuu na kupata matibabu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwa kweli kwenye eneo hili amekuwa akifuatilia karibu sana, lakini amekuwa akifuatilia sana wananchi wa kule Arusha kwa ukaribu sana hususani Karatu na amekuwa akinilitea wagonjwa wa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba inategemea unazungumzia Hospitali Binafsi kwa *level* gani? Maana yake ukiwa na Hospitali Binafsi ambayo *let say* ni *Polyclinic* na unazungumzia Muhimbili, bado bei haisababishi kuwa kubwa na vile vifaa na tiba yenyewe, maana yake kuna mambo mengi yanayozingatiwa kulingana na *level* ya hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge, nikimaliza kujibu swali tukae mimi na wewe unioneshe maeneo *specifically* ili nijue, tuangalie tatizo tulitatue kwa pamoja kwa sababu kwa kweli Hospitali za Serikali ndiyo inatakiwa iwe bei rahisi kuliko za *private*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kujua *specifically* ni nini, ili tuweze kushughulikia kwa pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kitu pekee ambacho kitaweza kutusaidia Watanzania kukabiliana na gharama kubwa za matibabu ni Bima ya Afya kwa Wote, lakini mpaka sasa mchakato bado unasuasua, Serikali haioni sasa ni wakati umefika wa kuwasaidia wagonjwa wetu hapa nchini kupunguza gharama ya usafishaji wa figo kutoka shilingi 300,000 mpaka shilingi 50,000? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza Mheshimiwa Kunti kwa swali hili zuri, lakini

ninakuhakikishia dada yangu, wiki hii ulimuona Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa Arusha na aki-*launch* programu kubwa sana ambayo sasa inaenda kuanza ya kuhakikisha Watanzania wote wanaenda kuingia kwenye Bima ya Afya kwa Wote ambayo ndiyo suluhu kubwa kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba Mheshimiwa Kunti, jinsi ambavyo anajipanga sasa hivi kurudi Bungeni, hivyo hivyo ninakuomba ujipange kuhakikisha wale wanaotakiwa kukurudisha Bungeni, wakati unawaambia nirudisheni Bungeni, basi nguvu hiyo hiyo utumie kuwashauri wakate kadi ya Bima ya Afya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia siyo tu suala la Bima ya Afya, ninazungumzia ku-*access* vifaa kutoka viwandani moja kwa moja, itashusha gharama za matibabu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Taska Mbogo, au swali lako limepita?

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, swali langu kidogo lilikuwa linafanana na la Mheshimiwa Paresso.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo limeshaulizwa?

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niliboreshe kidogo; gharama za kusafisha figo pale Muhimbili ambayo ni Hospitali ya Serikali ni shilingi 180,000 kwa *section* moja, lakini ili mgonjwa wa figo akae vizuri, anatakiwa kusafisha figo mara tatu kwa wiki, hii ni shilingi 540,000 kwa wiki. Kwa Mtanzania wa kawaida ni pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja yangu ilikuwa, ni lini Serikali itapunguza gharama za kusafisha figo kwenye Hospitali za Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mbunge kwa kweli kwenye eneo hili ninajua

anazungumzia, kwa sababu *physically* anajua anavyoniletea wagonjwa wenye matatizo yao, namna ya kusaidiana pamoja. Kwa kweli anafuatilia sana masuala yanayohusu watu kwenye eneo la afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwambia tu tumeanza, ndiyo maana ukienda baadhi ya hospitali sasa katika hospitali zetu za mikoa, hospitali mbili sasa za Mkoa wa Dar es Salaam tumefanikiwa kuhakikisha tunashusha na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri wa Afya sasa ameunda timu, inapitia kuja na *itemization* zote ili tujue tunapunguza wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unaweza ukapunguza, badala ya kupunguza ukaua mfumo wenyewe na kuua mfumo wenyewe unaweza ukasababisha watu wakose huduma kabisa. Ni bora wapate huduma kwa ghali, lakini waendelee kuwa hai wakati tunaangalia mambo yanakwendaje. Kwa kweli tunalichukua hilo, tunaenda kulifanyia kazi na timu imeanza kufanya kazi, wiki ijayo wanaleta ripoti watupe *way forward* ya kupunguza gharama.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Eric Shigongo. *(Makofi)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kuniona. Asilimia tatu mpaka saba ya watu wanasumbuliwa na tatizo la figo na miongoni mwa watu hawa ni watu maskini kabisa wasiokuwa na uwezo. Asia Mohamed anaishi bila figo kwa miaka 17 na wazazi wake wote hivi sasa wamefariki, ni yatima yuko kitandani anasubiri kifo.

Je, uko tayari Mheshimiwa Waziri, kusaidia binti huyu mdogo aweze kupata huduma ya kusafishwa figo ambayo ameshindwa kumudu tuweze kuokoa maisha yake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge, lakini nina mambo machache ya kumwomba; moja, kwanza ni kweli huyo dada amekaa miaka 17 akiwa na hilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, maana yake inaonesha ni kwa namna gani mifumo yetu ya afya ni mizuri kiasi kwamba mtu anaweza asiwe na figo, lakini bado akaishi bila kuwa na figo. Kwa maana ya kwamba anatibiwa vizuri kwenye hospitali zetu, wengine saa nyingine figo zina-*reject* mara nyingi, anarudiwa mara nyingi, lakini anaendelea kuwa salama na kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *issue* ni tunamsaidiaje? Kaka yangu Mheshimiwa Shigongo, pili ninakuomba suala siyo tutatibuje figo, suala ni kwamba tunakingaje watu wasipate matatizo ya figo, kwa sababu wewe ni mtu ambaye uko katika tasnia ya habari, ninakuomba pia utusaidie kutumia vyombo vyako vya habari ili kuhakikisha tunahamasisha elimu ya watu kuishi maisha ambayo hayatawasababisha wapate matatizo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Mbunge amlete huyo tutamfanyia *exemption*, ninaanza kwa kusema hapa miezi minne kwanza tutaanza naye atatibiwa bure wakati tunatafuta *solutions* zingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana. Aah, kuna swali bado, tuna muda kidogo.

Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mwenyewe vizuri kabisa kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Vijana wengi sasa hivi wanapata ugonjwa wa figo kwa sababu kuna pombe kali zenye sumu zimesambaa na zinauzwa kwa bei ndogo sana. Sasa kwa sababu umesema kinga ni bora, ni lini Serikali mnaanza *operation* mahsusi ili kuweza kuondoa pombe zote za aina hii Tanzania, ili tuweze kuokoa kizazi cha sasa na kijacho? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, uondoaji wa pombe kama ni kazi yako basi kama unaweza kulijibu, lijibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze tu Mheshimiwa Halima Mdee, wakati wote amekuwa

ni mtu mwenye uwezo wa kutafakari vitu kwa kina sana na kutazama kwa mapana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba ni kweli pombe zinasababisha matatizo mengi siyo masuala ya figo tu na hata wakati mwingine ukienda mezani ukisoma utaona mahali pameandikwa tumia pombe kwa akili, wengine anaandika matumizi ya pombe ni mabaya chini ya miaka 18 usitumie, hizo zote ni juhudi ambazo zinafanywa, lakini ni katika hali halisi ni masuala ya kubadilisha tabia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninawaomba kama ambavyo nimesema Wabunge wengi hapa sisi tuna *influence* sana, tutumie *influence* zetu kuhamasisha watu kwamba wanahitaji kuishi maisha salama hata kama kuna vitu vyenye madhara, lakini bado vinatumika, basi kila mtu awe makini kwenye kutumia. Ninachukua suala lako kwa sababu linahusu sekta mbalimbali, tuendelee kwa pamoja kushirikiana, tutaenda kushirikiana na sekta mbalimbali tuje na *way forward* ya pamoja ya kutoa hamasa kubwa kukinga hayo mambo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara nyingine, tunaenda Wizara ya Maji.

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

Nimwite sasa Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, aulize swali lake.

Na. 101

**Hitaji la Maji Vijiji vya Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza: -

Je, lini Vitongoji vya Kimele, Kilemela na Nyakahamba katika Kata za Mapinga na Kerege vitapata maji ya uhakika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitongoji vya Kimele, Kilemela na Nyakahamba ni kati ya vitongoji 15 vya Kata ya Mapinga na Kerege zinazopata huduma ya maji safi na salama kutoka chanzo cha Mtambo wa Ruvu nchini. Katika kuhakikisha huduma ya maji inakua ya uhakika katika vitongoji hivyo, Serikali kupitia programu ya *WSSP II* imetekeleza mradi uliohusisha miundombinu ya ulazaji bomba umbali wa kilometa 111.8 na ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 6,000,000 katika eneo la Vikawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo umeongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi wa Kata za Mapinga na Kerege hususani katika Vitongoji vya Kimele, Kilemela na Nyakahamba. Hata hivyo, kwa baadhi ya maeneo ya Kitongoji cha Kilemela kumekuwa na changamoto za kijiografia na kusababisha kutofikiwa na huduma ya uhakika. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali inatekeleza mradi wa kuongeza msukumo wa maji ili kupanua mtandao wa upatikanaji wa huduma ya maji katika kitongoji hicho, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mpo wengi kweli kweli. Mheshimiwa Shabani Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, nina maswali mawili tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyojibu kwenye jibu lake la msingi kwamba kuna mpango wa kuongeza usambazaji wa maji katika Kitongoji cha Kilemela, je, ni lini mpango huo utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kata ya Makulunge pamoja na Kata ya Fukayosi zinapata maji kutoka katika mtambo wa Wami. Vitongoji vya Engero, Mkwama, Kijiji cha Mkenge pamoja na Kitongoji cha Kalimeni wananchi wake hawajapata maji mwezi mmoja sasa, je, ni lini Serikali itarekebisha huo mtambo wa Wami ili wananchi hawa waweze kupata maji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri sana ambayo anaendelea kuifanya katika jimbo lake na kwa kuwasemea wananchi wake hasa katika sekta ya maji ameendelea kutupatia ushirikiano mzuri sana pale ambapo changamoto zinapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa upande wa Kibaha na Bagamoyo tumetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kupanua wigo wa kufikisha huduma ya maji safi na salama katika vitongoji. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, vitongoji ambavyo amevileta tutavifanyia kazi na tutaangalia namna ambavyo tutaenda kuvifanyia utafiti na kupata gharama halisi ili mradi uweze kuwafikia wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la mtambo ambao una changamoto, Serikali kupitia Wizara ya Maji tumeendelea kuhakikisha kwamba tunachukua hatua stahiki pale ambapo panatokea tatizo lolote lile katika mitambo yetu ili tuwe na uhakika wananchi wetu wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama na hayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hayo ni maelekezo ya Ilani yetu ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi kuhakikisha watu wanapata maji ya kutosha katika wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni lini Serikali itatatua shida ya maji Tarafa ya Wanging'ombe katika Jimbo la Wanging'ombe maeneo ya Saja, Kijombe na Kata ya Wanging'ombe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na pia nimshukuru sana Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge wa Njombe Viti Maalum kwa kuendelea na kazi

yake kubwa ya kuwasemea akina mama ambao ndio tunawapa kipaumbele katika kutatua changamoto za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaaomba nilipokee suala hili twende tukalifanyie kazi kwa sababu bado tunaenda kwenye bajeti ijayo ili tuone kwamba ni namna gani tutaweza kuliweka kwenye mpango wa bajeti ili tuweze kwenda kuchukua hatua ya kuwafikishia huduma ya maji safi na salama kwa kujenga miradi ambayo itawasaidia kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ningependa kufahamu, je, Serikali kupitia Wizara ya Maji haioni kuna uhitaji na sababu kubwa ya kuweka bei pungufu ya kuunganisha maji kama ilivyofanyika kwenye umeme kwa sababu nikitolea mfano kwenye Jimbo la Bukoba Mjini, Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kuna upatikanaji wa maji, lakini gharama ya kuunganisha wakazi ili waweze kunufaika na maji hayo bado ni kubwa sana.

Je, Serikali haioni ipo haja ya kuweka bei elekezi ambayo itakuwa ni gharama nafuu ili kuhakikisha kwamba kaya zote zinanufaika na maji safi na salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Neema Lugangira, anaendelea kuwasemea wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ina mambo matatu ambayo imejikita nayo; la kwanza, upatikanaji wa huduma bora, lakini pia muda wa upatikanaji wa huduma yenyewe, lakini na gharama ambayo mwananchi anatakiwa kununua huduma hiyo ya maji. Kikubwa ni kwamba Wizara yetu kupitia Mheshimiwa Waziri, alishatoa mwongozo na mwongozo huo ni kulingana na aina ya uzalishaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna aina ya maji ambayo tunayapata kwa njia ya mserereko, kuna aina ya maji tunayopata kwa njia ya umeme wa *solar* na kuna aina ya maji ambayo uzalishaji wake unatokana na umeme wa *TANESCO*. Kwa hiyo, ukiangalia uzalishaji wake na gharama zake zitakuwa tofauti. Kwa mfano, kwa sasa umeme wa *TANESCO* ndiyo umeme ambao uzalishaji wake unakuwa na gharama kubwa hivyo hata mtumiaji wa mwisho atapata kwa gharama kidogo ambayo imechangamka, lakini umeme wa *solar* kidogo inashuka kidogo, mserereko unakuwa chini kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ni nini? Kikubwa ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kupeana elimu ya kujua kwamba maji haya kuna gharama fulani ambazo zimehusishwa mpaka mtumiaji wa mwisho anaenda kuyapata hayo maji. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutaendelea kulitazama kama Serikali pale ambapo tutaona kwamba inaruhusu kupunguza gharama tutafanya hivyo kwa manufaa ya Watanzania, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali ya nyongeza jibu tu kifupi wataelewa. Tunaendelea, Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, Wilaya ya Ileje ina changamoto kubwa ya maji ikiwemo Kata ya Isongole na Itumba. Ninataka kujua ni lini mtapeleka fedha ili kumalizia Mradi wa Maji wa Isongole - Itumba na wananchi waweze kunufaika na maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa swali jema na zuri kwa ajili ya wananchi wa Ileje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea *exchequer* kutoka Wizara ya Fedha na tumeelekezwa kuleta madai ya wakandarasi mbalimbali ili waweze kulipwa ili miradi yetu iendelee kukamilika

na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Bahati Ndingo.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Kata yetu ya Mapogoro, Wilaya ya Mbarali ina uhaba mkubwa sana wa maji, nini mkakati wa Serikali wa kutanua Mradi wa Maji wa Nyaugenge na pia mkakati wa muda mfupi ili wananchi wa kata ile waweze kupata maji?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, ninakumbuka juzi alikuwa na mkutano wa hadhara katika jimbo lake na hoja hii iliibuka na sisi Serikali tumeshaipokea na tunaifanyia kazi. Wenzetu wapo kwenye hatua za manunuzi kumpata mkandarasi kwa ajili ya kwenda kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto hii ambayo imewakumba wananchi wake. Tuna jambo ambalo tunaenda kulifanya la dharura, tumeagiza *RUWASA* Mkoa wa Mbeya kwenda kufanya tathmini na kujiridhisha kama tunaweza kuchimba kisima cha dharura wakati tunasubiri mradi mkubwa wananchi wa pale waendelee kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ni mfupi maana bado ana swali la kujibu. Nimwite sasa Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 102

**Kukamilika kwa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria Rorya – Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, lini mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria wa Rorya - Tarime utakamilika kwa kuwa kasi ya utekelezaji ni ndogo sana?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Rorya - Tarime unaendelea kutekelezwa na Mkandarasi *CCECC* kutoka nchini China pamoja na Mtaalamu Mshauri *WAPCOS Limited* kutoka nchini India. Kwa sasa utekelezaji wake umefikia 13%, kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa tenki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita milioni tatu Mogabiri - Tarime Mjini; ujenzi wa tenki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita milioni moja Sirari na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji kinachojengwa eneo la Gamasara -Tarime Mjini. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Julai, 2025 na kunufaisha wananchi wapatao 729,496, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali kwa kweli hayana uhalisia kwa kutuaminisha wananchi wa Tarime na Rorya kwamba mradi huu utakamilika Julai, 2025. Mradi huu ulikuwa ni wa miaka mitatu, sasa hivi tunavyoongea imepita miaka miwili na nusu, fedha zimetolewa shilingi bilioni 21.9 tu *out of* shilingi bilioni 134 ambayo ni 16% tu, utekelezaji 13%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua mkandarasi huyo ali-*raise certificate* mbili; ya *1.9 billion* na *2.3 billion* nahisi wameshakuuliza hapa, zaidi ya miezi sita lakini mmetoa *1.9 billion* tu ndiyo maana amerudi *site* na hajarudi kikamilifu. Ni lini Serikali itamaliza kulipa ile *2.4 billion* ambayo *certificate* hii amei-*raise* zaidi ya miezi sita iliyopita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa sababu Serikali imeji-*commit* kumaliza huu mradi Julai, 2025 kwa hizo 86% kwa maana ya shilingi bilioni 112 zilizobaki na kwa sababu wamesema mradi huu unaenda kuwasaidia wananchi takribani 730,000, inatoa picha ni wananchi kiasi gani wanateseka hawana maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kupata *commitment* ya Serikali ni kwa jinsi gani wanaenda kutimiza ahadi hii kwa kutoa

hizo shilingi bilioni 112 ndani ya muda wa miezi sita ili mkandarasi huyu *CCECC* aweze kumaliza na kukamilisha mradi huu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na pia nimshukuru Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge ambaye amekuwa mstari wa mbele kuusemea sana huu mradi na ni hakika kabisa kwamba Serikali inasikia sauti ya Watanzania kupitia kwa Wabunge na inatambua kabisa kwamba mradi huu ni wa kimkakati. Ni kati ya miradi ya miji 28 ambayo Mheshimiwa Rais anaendelea kutuelekeza sisi Wizara ya Maji kuisimamia kwa weledi mkubwa na maarifa yetu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi kwamba ni lini italipa, kama ambavyo nimejibu katika majibu yangu ya msingi mkandarasi yupo 13%, alishalipwa takribani shilingi bilioni 22 na amesha-*raise* hiyo *certificate*. Tumemwomba arudi *site* wakati Serikali ikiendelea kuhakikisha kwamba ile *certificate* yake nyingine ambayo haijalipwa alipwe ili kuhakikisha kwamba mradi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu kwamba ahadi yetu ikoje kuhusu kulipa bilioni zote ambazo zimebaki, sisi kama Serikali tunalipa kwa mujibu wa hati za madai ambazo zitakuwa zinawasilishwa. Mkandarasi kila atakapokuwa anafikia hatua fulani na sisi Serikali tutakuwa tunahakikisha kwamba tunamlipa ili aweze kuendelea na mradi huo. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika na lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wa Tarime - Rorya wanapata huduma ya maji safi na salama kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie ndani ya muda wa mkataba tuna uhakika kwamba mradi huu utakuwa umekamilika bila ya kuwa na changamoto yoyote, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Dajameda pamoja na Kijiji cha Muungano, Kata ya Laghanga Jimbo la Hanang hakuna maji kabisa na wananchi wanatumia umbali wa kilometa 30 kwenda kata nyingine ya Bassotu kufuata maji, je, ni lini Serikali itawapelekea wananchi hawa maji?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Hanang ni kweli kabisa kwamba kuna changamoto katika vijiji hivyo pamoja na cha Muungano, lakini Serikali kupitia *RUWASA* tayari wameshafanya utafiti na wataanza kufanya usanifu wa kuvuta maji kutoka Bassotu kuja katika vijiji saba na katika hivyo vijiji saba ni pamoja na Kijiji cha Muungano na kijiji kingine ambacho amekitaja ambacho sijakisikia vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilikuona Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, suala la Tarime na Rorya linafanana na la Makao Makuu ya nchi. Je, ni lini Serikali italeta maji ya Ziwa Victoria Makao Makuu ya nchi Dodoma ili kuondoa adha ya ukosekanaji wa maji iliyopo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, katika mipango yetu ya kudumu ya kutatua tatizo la maji la Dodoma ni kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria, tayari Serikali imeshafanya *feasibility study* na sasa tupo kwenye *detailed design,* tukishakamilisha tunatafuta fedha na mradi huo unajengwa na Jiji la Dodoma linapata suluhisho la kudumu la changamoto ya maji, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laurent Kyombo, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali imetupatia Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kwa vijiji vyote vya Kata ya Kashenye na Kanyigo awamu ya kwanza na awamu ya pili itaenda Kata ya Bwanjai. Mradi huo mpaka sasa upo 92% lakini sasa hivi ni takribani miezi minne mradi huo umesimama.

Je, ni lini sasa Serikali itatupatia fedha ili kumalizia mradi huo na hiyo kiu ya wananchi wa Kata Kashenye na Kanyigo iweze kutimia mwaka huu wapate maji safi na salama?

**MWENYEKITI:** Majibu kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo kwenye mchakato wa kuhakikisha kwamba wakandarasi ambao wanasimamia miradi yote ya kimkakati wanalipwa ili waendelee na utaratibu wa kukamilisha miradi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ilitupa heshima Siku ya Wanamke Duniani kuchimba baadhi ya visima katika mikoa yetu na katika Mkoa wa Iringa ilichimba katika Kijiji cha Mtandika Sokoni na Kituo cha Afya cha Ruaha Mbuyuni, lakini mpaka leo hii hakijawekewa miundombinu yoyote.

Je, Mheshimiwa Waziri sasa upo tayari tukimaliza Bunge hili ukaweke miundombinu ili heshima ya mwanamke iwepo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Iringa nafikiri hili eneo lipo Kilolo, upande wa Mtandika visima vilichimbwa mwishoni mwa mwaka 2023, visima

hivi kimojawapo kiligundulika kuwa na chumvi nyingi sana. Mtandika tumetenga kiasi cha shilingi milioni 100, kwa ajili ya kwenda kumalizia, lakini kwa upande wa Ruaha Mbuyuni tuna mradi wetu wa mserereko ambao tunaandaa kufanya usanifu, ili twende kuhakikisha kwamba tunavuta maji, ili waweze kuhudumiwa na mradi mkubwa tofauti na mradi wa kisima ambacho kina chumvi nyingi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha Matondo, kwa kifupi tafadhali.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, je, ni lini Serikali itamlipa mkandarasi ili aweze kukamilisha Mradi wa Maji wa Vijiji Nane, Ukara katika Jimbo la Ukerewe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu - Wizara ya Maji, ameshawaelekeza *Regional Managers,* Wakurugenzi wa Mamlaka ambao wote wana madai ya wakandarasi kuyawasilisha Wizarani ili yaweze kuwasilishwa Wizara ya Fedha kwa malipo, ili waendelee na miradi ikamilike kwa wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, nimuite sasa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, aulize swali lake.

Na. 103

**Ujenzi wa Minara Katika Vijiji vya Arumeru Magharibi**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini minara itajengwa vijiji vya Kata ya Bwawani na Vijiji vya Nengung'u, Oloitushula, Olchorovus, Engutukoit, Losinoni Juu na Losinoni Kati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba yake, Mheshimiwa Maryprisca.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imekamilisha utekelezaji wa ujenzi wa minara mitano ya kufikisha mawasiliano ya simu katika Kata za Oljoro, Olmotonyi na Oldonyosambu zilizopo Wilayani Arumeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *UCSAF* itafanya tathmini katika Vijiji vya Kata ya Bwawani na Vijiji vya Nengung'u, Engutukoit, Losinoni Juu na Losinoni Kati ili kubaini mahitaji halisi ya huduma za mawasiliano katika kata hizo na kuweka mkakati wa namna bora ya kufikisha huduma za mawasiliano hitajika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Bwawani na Vijiji vya Nengung'u, Oloitushula, Olchorovus, kwa maana ya Kata ya Musa na Engutukoit, Losinoni Juu na Losinoni Kati, kwa maana ya Kata ya Oldonyosambu hawana mawasiliano, je, ni lini sasa Serikali itakwenda kuanzisha mradi huu kupitia *UCSAF* ili wananchi hawa wanaoteseka na mawasiliano waweze kuwa na mawasiliano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kufika katika maeneo haya, akapige simu ili ajionee changamoto hii wanayoipata wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Noah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kukupongeza sana Mheshimiwa Noah kwa namna ambavyo umeendelea kufuatilia suala hili. Tumeshaongea mara nyingi, lakini naomba nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi tayari wataalamu wetu wa *UCSAF* watakwenda kufanya tathmini. Hivyo mara baada ya ukamilishaji wa tathmini hii nikupe matumaini kwamba shughuli hii itaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutembelea eneo hili lenye tatizo la mawasiliano nipo tayari. Baada ya Bunge Mheshimiwa Mbunge tutawasiliana namna njema ya kwenda kufika katika eneo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Kijiji la Elerai katika Kata ya Olmolog, Wilayani Longido, wana changamoto kubwa ya mawasiliano. Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya kujenga mnara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimpongeze Mheshimiwa Zaytun Swai kwa swali lake na ufuatiliaji na yeye ni miongoni mwa Wabunge wanaofuatilia sana maeneo haya ya Longido. Nikutoe hofu Mheshimiwa Zaytun, kijiji hiki ulichokitaja na katika kata hii hapa Longido na yenyewe wataalamu wetu wanaendelea kuhakikisha mawasiliano yanapatikana ya uhakika wakati wote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, poleni sana, maana muda wetu umekwisha, tuna swali moja la kumalizia.

Kwa hiyo, tunakwenda kwenye swali la mwisho, Wizara ya Maliasili na Utalii. Nimuite Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

Na. 106

**Kutoa Ruzuku Vijiji Vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuanza kutoa ruzuku vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro kutoka kwenye mapato ya mlima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro inapakana na vijiji 94 vilivyopo katika Wilaya tano ambazo ni Moshi, Rombo, Siha na Hai, kwa Mkoa wa Kilimanjaro na Longido kwa Mkoa wa Arusha. Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro imeendelea kushirikiana na vijiji vinavyopakana nayo vikiwemo vijiji tisa vilivyopo katika Wilaya ya Hai kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa elimu ya uhifadhi ili kuwawezesha wananchi hao kunufaika kiuchumi na kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania hutekeleza sera ya kugawana faida zitokanazo na uhifadhi kupitia utaratibu wa Miradi ya Ujirani Mwema. Utaratibu huu unawezesha wananchi kuibua wenyewe miradi ya maendeleo na kiuchumi au kimazingira ambayo ni hitaji lao na kipaumbele, kisha hupeleka maombi hifadhini ambapo *TANAPA* huchangia 90% ya gharama ya mradi na wananchi huchangia 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya shilingi 90,550,000.00 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi minne katika Wilaya ya Hai. Miradi hiyo

itahusisha ukarabati wa madarasa manne katika Vijiji vya Foo, Nkuu Ndoo, Ng'uni na Saawe pamoja na mradi wa uwekaji wa mfumo wa gesi katika Shule ya Msingi Lukani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, niombe watekeleze ambayo wamekuwa wakiahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiuliza Serikali, kama ambavyo kwenye mashirika na taasisi nyingine wamekuwa wakilipa *CSR,* je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kubadilisha sheria na kanuni ili wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro waweze kupata *CSR* kama yalivyo maeneo mengine ya migodi na kwingineko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tayari tumeshaunda vikundi mbalimbali katika Jimbo la Hai kwa ajili ya kusaidia vijana wetu wanaopandisha wageni kwenye Mlima Kilimanjaro, lakini kumekuwa na tatizo, zile kampuni za watalii nyingi zinakuja na vijana wao kutoka maeneo mengine.

Je, Serikali haioni ni wakati sahihi sasa kuzielekeza kampuni hizi zichukue vijana waliopo pale *Machame Gate* na mageti mengine yaliyopo Mkoa wa Kilimanjaro ili vijana wanufaike na mlima wao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya kijamii imekuwa ikifanya vizuri isipokuwa tu baada ya tatizo la *Covid* ambalo mapato ya hifadhi zetu yalishuka ndipo miradi hii ilianza kupata changamoto. Baada ya mafanikio makubwa ya kudhibiti ugonjwa huu na kazi kubwa ya kutangaza vivutio vyetu vya utalii,

tumeona mapato yameendelea kukua siku hadi siku na tumeweka mfumo mahsusi kwa sasa unaotuelekeza kwenye kutekeleza miradi hii ya kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge katika bajeti ya mwaka huu tumetenga takribani shilingi 3,000,000,000 kwa ajili ya miradi hii ya kijamii. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge mtupe muda tuendelee na utaratibu huu wakati tunafanya tathmini ya mwenendo wa ukuaji wa sekta ya utalii ili tukiona imetengemaa basi tunaweza kuja na huo mpango ambao utapendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la ajira; suala la ajira kisheria ni fursa kwa Watanzania wote kuweza kufanya kazi mahali popote katika nchi yetu mradi hawavunji sheria. Sasa nimesikia changamoto hii ambayo Mheshimiwaa Mbunge ameisema, lakini tukumbuke vilevile kwamba ajira hizi zinatolewa na sekta binafsi na wao katika kutoa ajira hizi vipo vigezo, sifa ambazo wanaziangalia na kubwa zaidi kwao ni uaminifu kwa hawa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Hai kuona uwezo wa vijana wale, kama kuna mapungufu tupo tayari kushirikiana nao kuwajengea uwezo, lakini vilevile kuwahamasisha katika suala zima la uaminifu, ili tuhakikishe kwamba vijana hawa nao wanapata fursa ya kuajiriwa katika eneo lile na kuweza kunufaika na rasilimali iliyopo kwenye eneo lao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha maswali. Kuna wageni ambao wapo ndani ya Ukumbi wetu wa Bunge, ningependa niwalete kwenu.

Mgeni wa kwanza ni wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, huyu ni Paroko wa Parokia ya Minziro kutoka Mkoa wa Kagera, anaitwa Padri Dkt. Faustine Kamugisha, karibu sana, Baba Paroko. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, hawa ni viongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu kutoka Wilaya ya Ubungo, Mkoa wa Dar es Salaam. Hebu tuwaone mpo wapi? Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, Mbunge na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake wa Makundi Maalum, hawa ni viongozi wa *Jubilee Insurance Company* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge, huyu ni Mchungaji kutoka *Usa River,* Jimbo la Arumeru Mashariki, Mkoa wa Arusha, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge, huyu ni mpiga kura wake kutoka Wilaya ya Bahi, Mkoa wa Dodoma, ambaye ni Afisa Idara ya Uchumi, CCM Makao Makuu, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mbunge, huyu ni mama yake ambaye ameambatana na shemeji yake kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, karibu sana mama yetu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge, hawa ni wapiga kura wake kutoka Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge, hawa ni wapiga kura wake kutoka Tarime Vijijini, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge, hawa ni familia yake kutoka Pemba, Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni watano wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge, hawa ni vijana wa Taasisi ya *Youth Environment* kutoka hapa Jijini Dodoma, karibuni sana, wapo pale. *(Makofi)*

Tuna wageni 13 wa Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge, hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Chama cha Walimu Tanzania *(CWT)* kutoka Wilaya ya Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge, huyu ni muimbaji wa nyimbo za injili kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 13 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge, hawa ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana Wanamaombi. *(Makofi)*

Vilevile tuna wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, hawa ni Ndugu Martha Masanyika, huyu ni mjasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wanne kutoka Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya kutoka Jijini Dar es Salaam na Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Kipo kikundi cha wanawake 26 wa Kiislam wa Taasisi ya *Ladies in Islam Tanzania,* hawa wanatoka Dar es Salaam, Arusha na Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna walimu 14 wa Shule ya Msingi *Santhome Sabs Secondary School* kutoka Nala, Jijini Dodoma, karibuni sana walimu wetu. *(Makofi)*

Wanafunzi 113 na walimu 13 wa Shule ya Awali na Msingi *Mount Moriah* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana katika Bunge mjifunze. *(Makofi)*

Haya ndio majina ya wageni wetu kwa leo. Tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kuishauri Serikali kupitia michango yetu mbalimbali. Nina wachangiaji hapa na tutaanza na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na naomba nianze kwa kusema ninaunga mkono hoja na ninawapongeza wawasilishaji wote wawili, Waziri anayehusika na Mipango na Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuchangia kwangu nitakuwa ninagusa maeneo yote kwa pamoja na la kwanza, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi hii, lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya na

kazi kubwa ambayo imefanywa kwenye maeneo mbalimbali. Kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Profesa Kitila, maeneo mengi ambayo tumepata mafanikio makubwa kazi hii imefanyika vizuri katika kipindi cha muda mfupi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika maeneo ambayo yalikuwa yanatiliwa wasiwasi tayari Watanzania wamepata uhakika kwamba yataendelea kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia kuhusu umeme, tumesikia kuhusu reli, tumesikia kuhusu uwekezaji bandarini, naipongeza Serikali kwa kuendelea kusimamia vizuri ahadi ambayo tulitoa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mafanikio kwenye taarifa hasa ya Kamati kuhusu mafanikio hasa kwenye kilimo kwamba sasa tumefika takribani 700,000 kati ya hekta 1,200,000 zilizokuwa zimepangwa ambayo ni sawa na 60%. Kwa maoni yangu nadhani bado kilimo kama ambavyo tuliazimia kuongeza kutoka bilioni 270 na kitu kwenda trilioni 1.2 tunayo haja ya kuendelea kuboresha kilimo na kukipatia fedha nyingi za kutosha kwa sababu mpaka sasa bado ndiyo mwajiri mkubwa wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili nizungumzie *irrigation scheme* ambayo tayari mchakato wake ulikwishakamilika ya Ibanda - Igaka. Naipongeza Serikali kwa kukamilisha mchakato ambapo kazi hii ilikamilika tangu mwaka wa fedha ulioisha, lakini utekelezaji wa mradi huo haujaanza. Hii maana yake ni kwamba inawezekana pia Ibanda - Igaka ikawa ndani ya hizi hekta 727,000 ambazo kule kwetu sisi bado hatujaanza. Tunatakiwa kujenga kingio la maji halafu turekebishe lile eneo lenyewe la *scheme* ili hekta sasa hivi 2000 pale ziweze kuleta uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili kama Watanzania nadhani bado tunahitaji kutumia fursa ambayo tunayo. Tumezungukwa na nchi ambazo nyingine zina hali mbaya ya hewa, lakini tumezungukwa na nchi ndogo ambazo zinatutegemea sana kwenye mazao ya chakula na uzalishaji

wetu wa chakula pamoja na kujitosholeza sisi wenyewe ndani unatupa fursa ya kuuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaiomba Serikali kuweka fedha nyingi sana kwenye kilimo na kuzitoa fedha hizo kwenda kwenye miradi iliyokusudiwa. Tunatenga pesa nyingi, lakini zisipoenda ni sawa sawa na kujidanganya sisi wenyewe, tutakapokamilisha masuala ya *irrigation* na masuala ya uboreshaji wa mifugo ukienda vijijini bado wakulima wetu wanalima kizamani. Bado wakulima wetu *productivity* yao kwa heka ni ile ile ya mwaka 1960 wakati tunapata uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nitoe wito, nadhani ni vema tukaangalia namna ambavyo huduma za ugani zikawa *accessible* zaidi kuliko hata huduma nyingine. Tulikuwa na maadui wengi, tulikuwa na ujinga, maradhi sijui na nini, ukiangalia vizuri huko tumetoka, sasa tumebakiza umaskini na njia pekee ya kutoka kwenye umaskini ni kwenye kuboresha kilimo, kwa hiyo, nitoe wito kwamba maeneo haya yawekewe fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo imesemwa pia kwenye mifugo bado mchango wake ni mdogo, pia kwenye uvuvi bado mchango wake ni mdogo. Hapa kwenye uvuvi ninaipongeza Serikali kwa kutoa fedha nyingi kwenye vizimba *(cages)*. Ulikuwa ni ushauri wetu sisi kwamba tuache vizimba tuweke *cages,* lakini nadhani kuna *technical mistake* moja imefanyika hapo. Vizimba ni *very expensive,* lakini *running cost* ya kizimba kimoja mpaka samaki wakakue tangu kununua vifaranga na kuwanunulia chakula mpaka kukua ni kubwa, sasa Wizara ikaja tena na *proposal* ikapunguza kodi ya *importation* ya samaki kutoka nje, sasa matokeo yake hao wenye vizimba hawawezi ku-*operate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vizimba nataka nikuhakikishie vyote mlivyogawa ndani ya mwaka mmoja vitabaki kuwa *white elephant,* kwa sababu vyakula ambavyo vinapelekwa kwenye vizimba vinakuwa *imported* na vilivyopo Tanzania vinazalishwa kwa gharama kubwa, wakati huo kuna samaki wa bei rahisi sana kutoka nje ya nchi, sasa hili tuliangalie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye madini. Tunaipongeza sana Wizara ya Madini imefanya kazi vizuri hasa imechangia takribani 9% kwenye Pato la Taifa na imechangia kuingiza fedha za kigeni takribani dola bilioni 3.6, hili ni ongezeko kubwa sana.

Sasa Mheshimiwa Waziri wetu wa Mipango hapa nashauri jambo moja tu kubwa kabisa, ukiangalia vizuri mapato kwenye eneo hili makubwa yanatokana na wachimbaji wakubwa ambao wanachangia takribani 60% na wachimbaji wadogo 40%. Wachimbaji wadogo waliochangia 40% ya dola bilioni 3.5 bado asilimia kubwa wanachimba kienyeji. Mwaka jana tulipitisha pesa kwa ajili ya kuiwezesha Wizara kununua mitambo ya uchorongaji na kununua ndege, jambo hili lingefanyika haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, uwezekano wa siku moja tukawa na madini, lakini eneo lenye madini tukalikuta tayari ni vijiji au ni makazi ni mkubwa. Kwa hiyo, upimaji huu usipofanyika haraka na kwa sababu wenye ardhi ni wananchi tutajikuta tunayo madini chini ya ardhi, hatuwezi kuyachimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo tu, Dodoma hapa inawezekana kuna *gold* chini, lakini kwa sababu utafiti haukufanyika na mji unakua, kesho kutwa ukigundua kuna dhahabu ukiwa unaenda kule Mji Mpya wa Serikali, inaaminika kuna dhahabu, lakini tayari kuna mji pale chini. Kwa nini utafiti ulichelewa, watu wamejenga hiyo dhahabu haitachimbwa tena, kwa hiyo, tutakuwa na utajiri hapo chini ya ardhi ambao hauwezi kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninaiomba Serikali iharakishe utafiti kwenye eneo hili na utafiti ufanyike tuwe na *land bank* ya ardhi ambayo imefanyiwa utafiti wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye elimu; nimefanya utafiti tu mdogo nikagundua kwamba tuna tatizo kubwa sana, nadhani la vipaumbele. Miaka michache nyuma tulikuwa tunahamasisha wanafunzi au watoto kusoma sayansi na watu wengi sana wakaenda kwenye sayansi, sasa hivi kijana anamaliza *form six* anapata *division one* ya *PCB* ya *point* nane

mpaka *point* tisa anakosa chuo cha sayansi cha kwenda kusoma kwa sababu ushindani ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mifano karibu miaka mitatu yote ama minne. Mwaka juzi vijana wanne walipata *division one* ya *point* tisa, walikuwa wanataka kusoma *medicine*, *pharmacy* au *nursing* wakakosa chuo, wakaambiwa wasubirie mwaka unaofuata. Mwaka jana wakaamua kwenda kusoma biashara. Mwaka jana walikuwepo watatu wakakosa chuo, mwaka huu wakaenda kusoma biashara, mwaka huu karibu sita, Waziri wa Elimu anajua nilimwambia akiwa Geita. Huyu amefaulu *division one* ya *PCB* ambacho ndicho kipaumbele cha nchi, lakini vyuo hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unashindwa kuelewa, humu tunao maprofesa na madaktari ambao walikwenda *university* wakiwa na *division two* na wengine walikuwa na *division three* wali-*upgrade* wakaenda. Leo inakuwaje mtu wa *division one* ya *PCB* anakosa chuo eti *competition* ni kubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali haioni kwamba si una-*project?* Ni lazima u-*project* kwamba unajua *form six* wapo 120,000 kati yao wanaosoma sayansi ni 60,000, *tentatively* watakaofaulu ni 45,000, wewe wanafaulu wanapata *division one* halafu unamwambia huyu aliyehangaika na sayansi tangu *form one* mpaka *form six* aende akasome biashara, akasome sheria kwa sababu tu Muhimbili imejaa, *UDOM* imejaa basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye *enrolment* kwa mujibu wa taarifa hii ya *TCU* ya mwaka 2023 kati ya wanafunzi takribani 40,000 waliochukuliwa zaidi ya 20,000 ni vyuo binafsi. Ninaishauri Serikali hapa, tunapoteza vijana ambao wamepambana huku chini na tena wana uwezo mkubwa kwa kisingizio kwamba ushindani ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *imagine* mtu aliyepata *division two* wa *Art* anapata *course* yoyote anayoitaka, mtu aliyepata *division one* wa sayansi anakosa *course* aliyoikusudia kwa sababu Serikali haijajiandaa. Kwa nini Serikali isiongeze vyuo vya madaktari kama imegundua Muhimbili pamejaa, kama imegundua *UDOM*

pamejaa, kwa nini usipeleke chuo kikubwa katika kila hospitali kubwa ya kanda mkajenga chuo kikubwa cha Serikali cha *medicine*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kupelekwa na Bunge hili China sehemu moja inaitwa Nanchang, chuo kimoja kina wanafunzi 60,000 na *course* moja ina wanafunzi 30,000. Hapa sasa hivi wanakuambia chuo kimejaa, ukienda kuna wanafunzi 3,000. Tunawakatisha tamaa watu, sasa wote hawa tunawalazimisha kubadili *course* aliyokusudia kusoma, anakwenda kusoma *course* nyingine, matokeo yake hawa waliopo *form four* wote wana-*opt* kwenda kusoma *diploma*, matokeo yake sasa tunakuwaje? Matokeo yake huku mbele tunapokwenda tunaandaa kundi fulani hapa katikati ambalo na lenyewe litakuja na *crisis* kama tuliyonayo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo tumeshauri hapa sana kwa muda mrefu. Inawezekana mfumo hauna uwezo wa kugundua watu wenye matatizo au wenye shida ya mkopo. Mimi nina watoto ambao baba yake amefariki, cheti ameweka kwenye mfumo. Mama yake ni mama ntilie cheti ameweka kwenye mfumo. Mfumo unam-*reject* kwa sababu alisoma *english medium!* Sasa mwenye mkataba wa kuishi milele kwamba kwa sababu ulisomeshwa *english medium* huku chini au ulisoma *form four* ya *private* ni nani humu? Hebu tuambizane. Kila kitu ulichokitaka kwenye mfumo kimewekwa bado mfumo unasema *system* imem-*reject* kwa sababu huko zamani…, hebu tuwaambie Watanzania sifa hasa ni ipi ya kumsaidia Mtanzania. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu muda wako wa kuchangia umeisha na taarifa haiwezi kutolewa muda ukiisha. Naomba u-*wind up*.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie jambo moja tu. Ni haki ya kila Mtanzania aliyelipa kodi anapoomba mkopo apate mkopo, kama mfumo hauwezi kumgundua mhitaji, hakuna haja ya kuweka sasa *standards*

hapa, tuweke *flat rate* ili kila Mtanzania mwenye haki ya kusoma apate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nimuite sasa Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyopo mezani kwetu ambayo ni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo unaokusudia kutekelezwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa ushauri wangu kwenye mapendekezo ya mpango huu nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kushusha fedha nyingi sana za maendeleo katika Jimbo la Bukene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ninavyoongea jimboni kwangu Bukene kuna mradi mkubwa wa kusambaza maji ya Ziwa Victoria ambao una thamani ya shilingi bilioni 29, hii ni dhamira ya dhati kabisa ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kuondoa tatizo la maji ambalo kwa kipindi kirefu imekuwa ni kero ndani ya Jimbo la Bukene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongea sasa hivi jimbo langu lina mradi mkubwa wa *scheme* ya umwagiliaji ya shilingi bilioni 40 ambako tunakwenda kumwagilia zaidi ya ekari 4,000 za kilimo cha mpunga na hii inakwenda kuwa mkombozi mkubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Bukene hasa Kata ya Sigili, lakini tunakwenda kuongeza sana mapato kwa halmashauri kwa maana ya kupata mpunga mwingi sana kutokana na hii *scheme* kubwa ya shilingi bilioni 40 ndani ya Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo wote tunafahamu kwamba mradi mkubwa wa kusambaza umeme vijiji vyote ambao umegharimu shilingi bilioni 27 unakwenda vizuri na sasa

tunakwenda hatua ya vitongoji kwa vitongoji. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene tunatoa pongezi na shukrani za dhati sana kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mama Samia kwa namna ambavyo ametushushia fedha za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi sasa kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo huu ambao unakusudiwa kutekelezwa mwaka 2025/2026, kimsingi mapendekezo mengi ninakubaliana nayo isipokuwa nina ushauri kwenye maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo napenda kutoa ushauri, kwanza ninakubaliana na mpango kwamba kuendelea kujenga miundombinu muhimu ikiwemo reli ya kisasa *(SGR)* kwa sababu kile kipande cha *SGR* cha kutoka Tabora mpaka Mwanza kinapita katikati ya Jimbo langu la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu hapa ni kwamba tunapopanga bajeti ya ujenzi wa *SGR* tuzingatie sana *component* ya fidia. Sasa hivi kuna tatizo pale jimboni kwangu, nina watu karibu 183 ambao wametoa mashamba yao wamepisha ujenzi wa hii reli ya kisasa, lakini huu ni mwaka wa pili sasa, walishafanyiwa tathmini ikajulikana gharama wanayopaswa kulipwa kama fidia, lakini huu ni mwaka wa pili sasa hawajalipwa. Wananchi wameachia mashamba hivyo hawalimi na fidia hawajapewa na huu ni mwaka wa pili. Kwa hiyo, hii *component* ya fidia inaleta kero kwa wananchi wetu, mradi ni mzuri, faida za mradi ni nzuri, lakini sasa hii *component* ya fidia kidogo inaleta changamoto kwenye huo mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi 183 mashamba yao yametwaliwa kupisha tuta la reli, lakini mwaka wa pili sasa hawajalipwa, kwa hiyo, fidia ni jambo ambalo lizingatiwe sana tunapoweka bajeti ya miradi kama hii, *otherwise* miradi ni mizuri lakini sasa inakuja kuleta kero kama hawa wananchi wangu 183 wa Jimbo la Bukene ambao wanadai fidia mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa rai kwa Serikali kwamba wananchi hawa walipwe mapema sasa hivi hawawezi kulima

kwa sababu maeneo yao wametoa kwa ajili ya ujenzi wa reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kushauri kwenye huu Mpango wa Maendeleo ni kwamba nakubaliana na mpango kuweka kipaumbele cha kuendelea kufanya jitihada za makusudi za kuongeza tija kwenye kilimo. Ajira kuu au shughuli kuu ya wananchi wetu hasa sisi tunaotoka majimbo ya vijijini ni kilimo, kwa hiyo, ukitaka kuinua maisha ya wananchi wetu ambao wanajishughulisha na kilimo hakuna njia nyingine zaidi ya kuongeza tija kwenye kilimo. Sasa tija kwenye kilimo huwezi kukwepa matumizi ya mbegu za kisasa, matumizi ya mbolea za kisasa, matumizi ya huduma za ugani na haya yatawezekana tu kama Serikali itaendelea kuweka ruzuku hasa kwenye mbegu na kwenye mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu na ninapongeza jitihada kubwa za Serikali ambazo zimekwishafanyika kwa sababu maeneo mengi ambayo mbolea ilikuwa ikigharimu karibu shilingi 150,000 baada ya ruzuku ya Serikali imeshuka mpaka shilingi 70,000 lakini jitihada ziendelee kwa sababu maeneo mengi ya kwetu huko ardhi zimechoka, bila matumizi ya mbolea huvuni. Kwa hiyo bado kuna mahitaji makubwa sana ya matumizi ya mbolea na naunga mkono Mapendekezo ya Mpango ya kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea na mbegu bora ili wakulima wetu waweze kuongeza tija katika kilimo, kwa sababu ndiyo njia pekee ya kuongeza kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mapendekezo ya Mpango ya kuendelea kujenga *scheme* za umwagiliaji. Ili kuongeza tija katika kilimo lazima tulime mara mbili, lazima tulime kwa kutumia mvua za kawaida, lakini lazima tuwe na *scheme* za umwagiliaji ambazo zitatunza maji ili tuweze kulima kwa kipindi ambacho hakuna mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimboni kwangu kule sasa hivi kuna *scheme* zinaendelea kujengwa, lakini bado jimbo ni kubwa, vijiji vingi, kata nyingi, bado naishauri Serikali kuendelea kutenga fedha za kutosha ili tuwe na *scheme* nyingi zaidi za umwagiliaji. Kwangu kule na *scheme* za umwagiliaji za Kamanhalanga,

Kasela, Mambali, Itobo, Mwangoye na Chamipulu ambazo zikifufuliwa na kuboreshwa zitatufanya tuweze kulima kwa tija na kuongeza kipato kwa wananchi wetu ambao wengi wao wanategemea kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono Mapendekezo ya Mpango huu katika eneo la kuendelea kuboresha barabara zetu, barabara zetu hasa maeneo ya kijijini ni uchumi. Sasa hivi kuna jitihada kubwa ambayo inaendelea ya kuleta fedha kwa ajili ya barabara za kijijini na niipongeze *TARURA* kwa kiwango fulani wanajitahidi, lakini bado fedha inatakiwa iongezwe ili tuhakikishe barabara za vijijini zinapitika na mazao kule tunalima mpunga sana, mpunga uweze kubebwa kwa gharama nafuu kwenda kwenye maeneo ya masoko.

Kwa hiyo, naunga mkono eneo la mpango ambalo linasisitiza Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha barabara hasa za vijijini ili kuongeza tija katika kilimo na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia umeme vijijini kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao *(value addition)*. Hapa ushauri wangu ni Serikali sasa baada ya kueneza umeme vijiji vyote, umeme huu sasa uende ukatumike kuongeza thamani ya mazao na wakulima ambao walikuwa wanauza mpunga, sasa wasiuze mpunga wauze mchele, wakulima ambao walikuwa wanauza alizeti zikiwa ghafi sasa wawe na viwanda vidogo vidogo na wasindike mafuta ya alizeti ili wauze mafuta ya alizeti badala ya kuuza alizeti yenyewe ghafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ninashauri jitihada za makusudi zifanywe ili vikundi vya wakulima kule maeneo ya vijijini wafundishwe na wapewe mitaji ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo ambavyo vitaongeza thamani ya mazao kwa makusudi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Bukene kule tuna maembe mengi mno, tunalima maembe mengi. Hakuna sababu yoyote ya wanavikundi eneo la kwangu kule kushindwa

kuungana na baadaye Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi wa Taifa kuwasaidia mitaji ili waweze kuwa na viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda kwa kutumia maembe ambayo wanalima kule. Kwa hiyo, kuwe na jitihada za makusudi za Serikali za kuwawezesha hawa wakulima ili sasa waongeze thamani ya mazao yao ili waweze kupata tija kwenye maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kabisa Serikali iliamua kuweka maeneo ya *EPZ* kwa ajili ya maendeleo na kuhakikisha kwamba uchumi unakua kwa kasi. Katika maeneo 17 ambayo yalitengwa, ni mawili tu ambayo ni pale Benjamin Mkapa na Bagamoyo ndiyo ambayo yameweza kufanya kazi na mengine yote bado fidia na vitu kama hivyo vinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwamba shilingi bilioni 9.9 imeanza kulipwa kwenye fidia, lakini maeneo ya Nala hapa Dodoma na kule Songea, bado. Tunafikiri kwamba tunapokuwa na mipango na tunapoenda kufanyia, kazi basi tuongeze *speed* na ndiyo maana wenzangu wametoka kusema hapa, watu wanaachia maeneo kwa ajili ya kupisha Serikali ifanye maendeleo, lakini Serikali inakaa muda mrefu sana bila kuwalipa fidia ili kusudi watu waendelee na maisha yao na kwamba ile mipango ambayo Serikali imepanga basi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatambua kwamba hiyo shilingi bilioni 9.9 ni ndogo, watu wengine bado wanadai. Kama nilivyosema hapa Dodoma tumesema ndiyo jiji na ndiyo katikati

ya nchi na ni makao makuu, basi walipe pale Nala na kule Ruvuma ambapo tayari ndugu zetu wameachia maeneo kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kabisa ili kujenga mpango wa mbali ni lazima nguvu ya kiuchumi ya wananchi iendelee kuwepo. Leo hii tuna Mfuko wa Barabara, tunapopata hela katika mfuko ule basi pesa zitoke mapema ili kurekebisha maeneo yaliyoharibika au kujenga barabara zingine. Tunaomba Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mwigulu nafahamu yeye anajua, tusipofanya hivyo basi barabara ambayo inabeba hayo mazao ambayo watu wetu wanalima huko inaweza ikaleta bei ya mazao kuwa kubwa zaidi kwa sababu ya usafirishaji kuwa mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua *SGR* imefanya vizuri, *TAZARA* najua sasa hivi wana mazungumzo kwamba angalau wenzetu wa China walioitengeneza warudi na kuisimamia. Kwa sababu *TAZARA* ilikuwa inasaidia sana Nyanda za Juu Kusini kwa ajili ya kubeba mazao na pia kusaidia usafirishaji, basi tunaomba mazungumzo hayo yafanyike haraka na *TAZARA* irudi kwenye nafasi yake ya awali ili watu wa Nyanda za Juu Kusini tuweze kufanikiwa tukitambua kabisa kwamba sisi ndiyo wazalishaji wakuu na mazao mengi yanatoka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia habari ya TEHAMA; TEHAMA ni kitu muhimu sana kwa sababu Tanzania haijajitenga. Tunaamini kwamba tusipokuwa na mifumo ya kitaalamu kama hiyo basi tunafanya watu wetu kurudi nyuma hasa katika mambo ya kiteknolojia. Tunaomba fedha iongezwe kwa hawa ndugu zetu wanaoshughulikia TEHAMA ili tupate wataalamu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba kuna akili bandia ambazo zinatakiwa kuongezeka vyuoni kwa ajili ya kusaidia ufundishaji wa wataalamu mbalimbali. Basi tunaomba tuwekeze huko ili na sisi twende kwa *speed* kubwa sana ya kimaendeleo, kwa maana ya TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunazungumzia habari ya minara. Tumesema hapa na tumesikia kwenye bajeti zilizopita

kwamba tunahitaji kuwa na minara zaidi ya 758, lakini mpaka sasa ni minara 295 tu iliyojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba tunapokuwa na teknolojia ya habari au kupata simu kwa watu wa vijijini ni kitu muhimu sana katika kuleta maendeleo. Leo hii wakulima wanatafuta masoko kwa kutumia simu. Pamoja na hayo, Maafisa Ugani ni wachache, kwa hiyo, wanaweza wakatumia teknolojia ya simu kuweza kuendeleza wakulima wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba minara vijijini iongezeke, kuna maeneo mengi sana, kwa sababu kati ya minara 758 iliyojengwa ni minara 295, kwa hiyo haijafika nusu. Tunaomba *speed* iongezeke ili tuweze kuwa na usikivu mzuri sana wa simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tunaomba tufanye angalau *bundle* na gharama za simu zishuke kidogo. Hii itasidia watu wa vijijini hususani wanawake kuweza kuwa na mawasiliano na wakaingia katika mambo ya simu kwa kuwa itakuwa ni bei rahisi kudogo, lakini tunapokuwa na *bundle,* unaweka *bundle* limeisha na hatujui limeishaje na kampuni za simu lazima zidhibitiwe ili tuweze kuona watu wetu wakifanikiwa katika uanzishwaji wa simu na kuongeza idadi ya watumiaji wa simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa kwamba ili tuweze kuendelea, bado ile kauli ya kwamba kilimo ni uti wa mgongo, mimi nniaamini bado inaendelea. Ninajua kwamba Mheshimiwa Kitila anayafahamu mambo haya. Sasa basi, watu wengi ambao wako kwenye kilimo, ni kweli bajeti imeongozeka kwenye kilimo, tumetoka mbali na sasa tuna *1.2 billion* kwenye bajeti yao, tunawashukuru kwa kuongeza, lakini bado lazima tusimamie kilimo kwa sababu watu zaidi ya 70% wako kwenye kilimo. Tunajua kabisa kuwa mbolea inatoka, lakini je, inatoka kwa wakati? Wale wanaopewa dhamana ya kuendeleza mbolea za ruzuku ni waaminifu? Usimamizi lazima uwepo na ni lazima tuwekeze kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Chuo cha Kilimo Uyole kwa muda mrefu sana hakipati fedha za utafiti. Tutapataje mitambo mizuri tusipowekeza kwenye watafiti? Tunawezaje kuwa na mbolea ya kufaa bila kuweka watafiti wa kujua kwamba mbolea hii itafaa. Tunafahamu kabisa leo hii kumekuwa kuna watu wanauza mbegu *fake,* tunahitaji watafiti ambao wataisaidia Serikali kusema kwamba mbegu hizi hazifai, tunahitaji mbegu hii. Tunaomba sana sana muongeze jitihada katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa tunavuna, leo hii tuna parachichi ambayo tunaiita ni dhahabu ya kijani. Ni kweli imepanda katika soko la nje, lakini tunahitaji kuongeza nguvu ya bei ya parachichi na kuwaondoa madalali wanaowaumiza wakulima. Leo hii mkulima analima parachichi halafu anakuja dalali anasema parachichi hii ni *reject*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuongeze wataalamu kule chini ambao wataweza kuwasaidia wakulima waweze kuuza parachichi zao. Kwa sababu yanakuwa *reject* kwa macho ya nani? Anasema *reject* halafu anayachukua, halafu yeye anakwenda kuyauza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali isimamie hilo na tunapoendelea na mipango hii ni lazima tuwalinde wakulima hawa kwa sababu zao la parachichi haliishi leo. Tumeona kwamba parachichi siyo tu chakula, ila inatengeneza pia dawa pamoja kusaidia mambo tofauti. Kwa hiyo, mimi ninaomba katika mpango wa kilimo tuhakikishe tunatumia muda mrefu sana, kuweza kulilinda zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inakwenda sambamba na zao la chai. Tunafahamu kwamba chai inanyweka dunia nzima. Leo hii wanasema kwamba soko la chai limeshuka, siyo kweli. Kati yetu hapa wote tunakunywa chai na dunia nzima inatumia chai. Basi tupambane kwenye soko la dunia ili chai yetu iweze kusonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wawekezaji wanaotoka nje ni lazima tuwangalie kwa jicho la *forensic*. Haiwezekani mwekezaji anatoka nchi za *East Africa* hapa, nchini kwake analima chai na

wala kiwanda hakifi, lakini akija kununua kiwanda na kuwekeza hapa Tanzania, anafunga kile kiwanda anasema chai haina soko, lakini hapo jirani tu anapotoka yeye huyo mwekezaji chai inaendelea. Kwa hiyo, tunawaomba watu wa usalama wasimamie, wahakikishe chai ya Tanzania inapata bei kama ambavyo *East Africa* wanauza kwa bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa kuwa ili uwe na mpango mkubwa wa muda mrefu na mzuri basi watoto wetu tuwapatie elimu nzuri na kwamba tuhakikishe kuwa wanakuwa na elimu ambayo inaeleweka. Tunaomba Wizara ya Elimu ihakikishe kuwa mitaala yetu haichezewi wala kubadilika badilika kila wakati. Tuhakikishe kuwa watoto wetu wanapo-*stick* kwenye elimu fulani ambayo Bunge na wananchi kwa pamoja tumepitisha, basi iende hivyo. Isiwe kwamba leo *GPA*, kesho wanatoa na kufanya kitu kingine, huko ni kuyumbisha wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja na ninaamini tutatoa mpango ambao ni mzuri wa kulisaidia Taifa letu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakagenda. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai na kusimama hapa mbele yenu. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa miradi yote ya maendeleo ambayo imekamilika na kwa miradi ambayo inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Profesa Kitila

pamoja na Mheshimiwa Dkt. Nchemba kwa mambo yote wanayoyafanya pamoja na Wizara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kupongeza kwa upande wa mambo ya vipaumbele. Vipaumbele vingi ambavyo wameviweka na mpango uliotimilika kweli ni mzuri, hata hivyo nitaweza kuongea kwa kiasi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naongea kuhusiana na kipaumbele cha miundombinu pamoja na usafirishaji. Hapa nitaongelea hasa kwenye upande wa reli hii ya mwendokasi ambayo tayari inafanya kazi kwa kuanzia Dar es Salaam mpaka Morogoro kilometa 300 na kuanzia Morogoro mpaka Dodoma ambapo Waheshimiwa Wabunge na watu wengi wanasifia na wote tunaitumia kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande ambacho kitawekwa kwenye mpango ambacho kinaendelea kujengwa ni kipande cha kuanzia hapa Makutupora kuendelea mpaka Tabora na kipande cha awamu ya pili ni kuanzia Tabora kwenda mpaka Kigoma mpaka Kalema. Kwa hiyo, mpango huo uwekwe na huo mradi uweze kukamilika kwa wakati kama utakavyokuwa umepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye mpango huu, ninaomba uhusishe treni ya mizigo kwa sababu treni ya mizigo ya *SGR* itasaidia sana. Ninasema hivi kwa sababu tumejenga barabara, lakini zinaharibika kutokana na mizigo mikubwa ambayo inabebwa na malori. Kwa hiyo, kwa tutumie treni ya mizigo kwamba ninashauri iwekwe kwenye mpango, ionekane, itekelezwe na iweze kufanya kazi kwa wakati. Hiyo itakuwa imesaidia sana kwa upande wa usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara, ninaungana pamoja na mpango kuwa barabara ziunganishe mikoa kwa mikoa na barabara za mikakati. Hapa ninaongelea kwa Mkoa wangu wa Morogoro ambao ninashukuru na kuipongeza Serikali ambayo imeanza matengenezo ya barabara inayoanzia Kidatu kwenda mpaka Namtumbo – Songea. Pia kwenye mpango huu ninashauri kuwa iweze kuwekwa vizuri ili

kuweza kukamilika kwa wakati kwa sababu inasaidia kwa pande mbili za Ruvuma pamoja na Mkoa wa Morogoro kwa kukuza uchumi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye upande wa vipaumbele ninakwenda kwenye sekta ya uzalishaji. Ninashukuru kwenye mpango wameweka sekta za uzalishaji, lakini ninaomba ikaziwe kabisa hasa kwenye upande wa kilimo, mifugo pamoja na uvuvi ambao unaleta uchumi na kuongeza Pato la Taifa pamoja na la mkulima na kumwezesha mkulima huyo kuwa na hela kwenye mifuko yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo, ninashauri mpango uweke na msisitizo sana kilimo cha umwagiliaji. Kwa mfano, ukija kwenye *central corridor* (Ukanda wa Kati) unakuta kuwa mara kwa mara ni kame. Kwa hiyo, hii mipango ihusishe sana uchimbaji wa mabwawa ili waweze kumwagilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninapongeza kwa upande wa Mkoa wangu wa Morogoro kwa kuwa tuna maji ya kutosha, lakini ninashauri *schemes* za umwagiliaji ziweze kuendelea. Hii ni kwa sababu Mkoa wetu wa Morogoro tunaweza tukalisha nchi nzima kwa kuwa ni mkoa ambao una udongo mzuri na una maji ya kutosha. Hata hivyo kilimo cha umwagiliaji ndicho kinachoweza kikaturudisha wananchi nyuma kwa ujumla. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kuwa iweze kuendelea hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru na kuipongeza Serikali na mpango mzima. Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kutoa ruzuku ya mbolea na ruzuku ya mbegu ambazo sasa hivi inasaidia wananchi kwa sababu wanapata mbolea pamoja na mbegu kwa upande wa ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza hivyo na tukipata maji kwa ajili ya umwagiliaji, mbolea pamoja na mbegu ajira itapanda, Pato la Taifa litaongezeka na pato la mwananchi litaongezeka. Kwa hiyo, mpango huu ukazie sana kwenye kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee upande wa viwanda na kuthamanisha vyakula. Ninaomba sana kodi iangaliwe kwenye viwanda, utitiri wa kodi, ukubwa wa kodi na ongezeko la kodi. Unakuta viwanda vingine vinashindwa kujiendesha kwa sababu kodi zinakuwa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mpango huu uweze kuendeleza na kujenga viwanda huku tukiwa tunaongeza viwanda, tuweze kuona viwanda hivi hasa vitakavyoanzishwa hapa na kuweka mazingira mazuri ya wawekezaji ambao watakuja kuwekeza kwenye viwanda hasa katika kuongeza thamani ya vyakula kwa kutumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini. Kwa namna hii tutaweza kuongeza ajira pamoja na kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vilivyokufa, kwa hiyo, ninashauri mpango huu uangalie kwamba je, viwanda vilivyokufa, vinafufuliwaje na vinaendeleaje? Hapa naweza kuipongeza Serikali kwa mpango uliopo wa kukifufua na kukiendeleza Kiwanda cha Mang'ula Kilombero ambacho kitafufuliwa na kitandelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuendelea kuongea kuhusu mpango wa miradi ambayo haijakamilika. Hapa pia ninamaanisha na miradi ya maji ambayo haijakamilika, maboma ya madarasa pamoja na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuanzisha mipango mipya mpango huu ujikite kwenye kumalizia mipango viporo ambayo bado hajamalizika. Hapo ninagusia pia Mradi wa Liganga na Mchuchuma, ni mradi wa miaka mingi sana, nilianza kuusikia Mradi wa Linganga na Mchuchuma kwa miaka mingi na mimi mwenyewe nimetembelea huko miaka ya nyuma. Kwa hiyo, ninaomba mradi huu umalizike ili tuweze kupata chuma cha kutengeneza mambo yetu ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuitilie maanani Liganga na Mchuchuma kwenye mpango huu ili mradi uweze kukamilika. Kama tatizo ni mkandarasi aweze kuangaliwa. Kama tatizo ni mipango iangaliwe ili kusudi nayo iwe historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bwawa la Mwalimu Nyerere; Bwawa la Mwalimu Nyerere linaendа vizuri, ninashukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu umeme sasa unaanza kutoka na unaendelea vizuri ingawa ni *lots* chache, lakini ikifikia *lots* tisa zote ninaamini tutapata umeme wa kutosha, tutaweza kuanzisha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa na pia tutaweza kuuza nje na kupata fedha za kigeni kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niangalie upande wa maliasili, mazingira na tabianchi. Hapa ninaomba kwenye mpango wetu tuiweke kuwa huu mfuko ambao tunausemea uweze kuona kuwa kama Serikali tunaiongezeaje hela na ni mikakati gani tuchukue kwa ajili ya kutunza mazingira yetu. Kwa sababu hili ni janga kubwa la Taifa kama tutaacha mazingira yetu yakaharibika. Tutapata joto la kutosha na tutakosa mvua, yaani kwa kweli itakuwa ni *disaster* kubwa sana. Kwa hiyo, tuweke kwenye mpango jinsi ya kutunza mazingira, jinsi ya kupanda miti na jinsi ya kuiendeleza nayo itakuwa imekuwa nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wazabuni, wakandarasi pamoja na watoa huduma, ni kweli kwenye mpango wanasema kuwa wamelipwa, lakini siyo wote. Ninaomba huo mpango uangaliwe ili wale ambao hawajalipwa wawekwe kwenye mpango ili waweze kulipwa kwa sababu kama hatutawalipa, tunachelewesha ile miradi kukamilika kwa sababu huyo mzabuni, mkandarasi hawezi kuendelea bila kupata hela ya kulipwa. Kwa hiyo, ninaomba sana hiyo nayo tuiangalie. Huo ni ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naongelea kuhusu maji. Maji ni maji na kila mmoja anataka maji. Kwa hiyo, mipango ya maji naomba tuiangalie, vile vijiji vyote ambavyo havijapata maji wananchi waweze kupata maji na fidia ziweze kufidiwa. Kwa mfano, wakulima wangu na wananchi wangu wanaozunguka Bwawa la Mindu hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namalizia kuwa umeme upelekwe vijijini na kwenye vitongoji ambao hawajapata. Ahsante sana kwa kunipa nafasi na ubarikiwe na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ahsante sana kwa mchango wako. Nimwite sasa Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja zilizopo mezani kwa maana Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2025 na Mwongozo wa Bajeti ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia maono yake na kwa kusimamia mpango ambao tunaenda kuumaliza wa mwaka mmoja na kuja na mpango mzuri huu ambao unatuonesha mwelekeo wa kuweza kuleta maendeleo zaidi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika Mheshimiwa Rais katika mwaka mmoja huu ambao tunaumaliza amefanya kazi kubwa sana. Sisi ambao tupo majimboni tumeona fedha nyingi zimekuja kutekeleza miradi ambayo ilikuwa kwenye mpango uliopita. Kwa hakika wananchi katika maeneo yote wanampongeza Mheshimiwa Rais na wanamshukuru kwa sababu kuna maendeleo makubwa. Fedha zimekuja nyingi, miradi imekuwepo ya kutosha, miradi ya elimu, afya, barabara, umeme pamoja na aina mbalimbali ya uwezeshaji katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili Mheshimiwa Rais amefanya jambo jema na sisi tunampongeza sana kama Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Mipango pamoja na Uwekezaji ambaye kwa kweli wamefanya kazi kubwa kuandaa mpango huu. Pia tumpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kutuletea Mwongozo wa Bajeti ambao Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba pamoja na Waheshimiwa Naibu Mawaziri wao wamefanya kazi kubwa ambayo tumeiona hapa na imetupa mwelekeo mzuri wa kuweza na sisi kuongeza ushauri katika mpango waliotuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mpango huu tumesoma na tumeona kwamba uchumi umekua kwa maana ya Pato la Taifa limekua katika kipindi hiki. Kwa hakika tunajivunia sana kwa sababu mipango ambayo imetekelezwa imesababisha uchumi kukua. Kwa hiyo, kupitia taarifa tuliyosomewa hapa inaonesha mwelekeo wetu ni mzuri na uchumi wetu ni stahimlivu ambao kimsingi tukiendelea kufanya mipango tuliyosomewa leo tunaweza tukaja mwakani na uchumi wa juu zaidi tofauti na mwaka huu ambao tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Ninataka kusema kwamba Pato la Taifa tumeelezwa hapa limekua kwa wastani wa 5.1% ambayo kimsingi ukilinganisha na mwaka ule uliopita wa 4.7%. Haya ni mafanikio makubwa ambayo kwa kweli yanaleta matokeo makubwa ya uchumi wetu. Hili tunaweza kuwapongeza Waheshimiwa Mawazari kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pato la Taifa linategemewa kukua mwaka 2025 kufikia 5.8% lakini mwaka 2026 kufikia 6.1%. Ni jambo kubwa la kupigiwa mfano, tuwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kufanya kazi nzuri pamoja na wataalamu kusimamia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili pato hili limefikia hapa ni baada ya kuwekeza kwenye miundombinu ya nishati na usafirishaji, lakini pia mmeongeza mikopo ya sekta binafsi na jitihada za kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara katika nchi yetu. Haya ni mambo ambayo mliyafanya, lakini pia utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya kilimo *(ASDP II)* ambayo tunaendelea kutekeleza mpaka sasa. Kipaumbele cha Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa Miaka Mitano 2021/2022, 2025/2026 ilieleza ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili kama ambavyo tumesema tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini niseme tu kwamba tunayo kazi ya kufanya ya kuhakikisha kwamba tunaongeza nguvu kubwa. Tupongeze sana kwenye hatua ya kuwa na nishati ya uhakika, eneo hili tulikuwa na tatizo

kubwa la kukatika umeme, kuwa na mgao nchi nzima. Leo tunapoenda kumaliza ule Mradi wa Mwalimu Nyerere tunaenda kuleta megawati 2,115 kwenye Gridi ya Taifa, ni jambo kubwa katika nchi. Tunategemea kwamba tutakuwa na umeme wetu huu unaotosheleza, lakini tutakuwa tunauza nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili, hiki ni kivutio kikubwa cha uchumi na ni kivutio kikubwa cha uwekezaji. Mwekezaji akija nchini lazima aulize kwanza tunayo nishati ya kutosha? Kwa hiyo, kwenye hili sisi tume-*win* na ndiyo maana unaona wawekezaji wanakuja, ni kivutio kikubwa. Tunaipongeza sana Serikali, tunaomba muendelee kusimamia vizuri mipango hii. Tumesikia juzi *SONGAS* mmeshamaliza nao mkataba wa miaka 20, maana yake sasa hatutakuwa na sababu ya kugawa fedha kwenye maeneo mengi. Kwenye hili tuipongeze sana Serikali kwa hatua kubwa ambayo mmeifanya. Tunaenda kuwa na umeme wa uhakika kama ambavyo tulikuwa na ndoto kwamba tutakuwa na umeme wetu na tutauza nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili tupongeze mradi wa *SGR,* tumeshaona matunda yake. Juzi tumepewa takwimu na Mheshimiwa Waziri husika wa Sekta ya Uchukuzi kwamba tumepata faida kubwa katika muda mfupi ambayo kimsingi pato lile linaenda kuongeza uwezo wa Serikali kuhudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili niombe sana juhudi ziendelee na katika mpango huu tumeona kuna mpango wa kumalizia vipande vingine. Kwa hiyo, niombe juhudi ziendelee, tuendelee kumalizia vipande vilivyobaki kutoka hapa Dodoma kwenda Tabora, kutoka Tabora kwenda Isaka kule Mwanza na baadaye twende mpaka Kigoma kabla hatujaenda nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tukiwa na uwezo mkubwa wa kusafirisha abiria na bidhaa, tutasaidia kuongeza uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, niombe sana eneo hili kwa sababu tunaboresha bandari yetu, kwa hiyo, *SGR* itakuwa na jibu la kupeleka mizigo katika nchi za jirani kupitia treni yetu ya mwendokasi ambayo tunaisema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili tumewekeza sana vizuri kwenye eneo la elimu pamoja na afya (huduma za wananchi). Tumefanya kazi kubwa, maeneo mengi tumeona maboresho makubwa. Kwenye Sekta ya Elimu tumejenga madarasa, tumejenga maabara za kutosha, tumejenga maeneo mengi na tumejenga mpaka matundu ya vyoo ambayo ilikuwa ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, leo tuna changamoto kidogo ya mabweni ambayo tunatakiwa tuongeze nguvu sana ili tuweze kujenga mabweni, watoto wetu waweze kuwa na mazingira mazuri ya kujifunzia. Pia kwenye eneo hili tuhakikishe tunajenga nyumba za walimu. Walimu hawana nyumba za kutosha, katika maeneo mengi walimu wanakaa mbali na eneo la shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana mpango unaokuja uweze kutusaidia kuleta jibu la kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira mazuri ya walimu wetu. Kwenye eneo hili tumejenga barabara vijijini zimefunguka. Maeneo mengi wananchi wanafurahia kuona miundombinu yao, wanasafirisha mazao yao na wanasafiri kwenda hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili tuongeze nguvu, bado barabara nyingine hatujamaliza, madaraja tumalize ili wananchi wetu waweze kufurahia mipango ya Serikali na kuhakikisha kwamba wanaongeza uchumi wao kwani uchumi huo ambao tunausema wa kuchochea uchumi shindani na shirikishi ni pamoja na kuboresha mazingira kwa wananchi kufanya shughuli zao na zaidi tuongeze kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa mud awa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu muda wako umekwisha.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, niombe sana kwenye eneo la uchumi wa wananchi tuongeze juhudi za kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uchumi wa wananchi mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja iliyopo mezani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu nakushukuru sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii na ni *saada* na *soud* mimi kupata ridhaa ya Mwenyezi Mungu kusimama hapa ili kutoa mapendekezo yangu katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mwenyezi Mungu, tunamshukuru Mheshimiwa Rais na tunashukuru watu wote wa Wizara zote mbili kwa maandalizi ya mpango mzuri, kitabu hiki kizuri, tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushie mabalaa na majanga haya yaliyokuwepo humu basi yaweze kufanyiwa *implementation* kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema mara kadhaa kwamba maendeleo ni mchakato na mimi hapa uniruhusu kidogo niseme maana yake nimeona kuna mzee mmoja huko nje anazungumza Bunge hili ni Bunge la kusifia sifia na kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasifia na kupongeza kwa sababu yapo mambo tumeyaona katika mpango wa mwaka jana na mpango wa mwaka juzi katika nchi yetu yametokea. Mara zote tumekuwa tukisema hapa tunalalamika, tunasema mambo ya maendeleo ya watu wetu. Sasa leo tunavyotoa mifano na vitu unavyoviona na Mheshimiwa Rais anavyozunguka, anavyoenda kusema kuhusu vitu hivyo anavyovifungua hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Jimbo la Kilombero tumepata Kiwanda cha Sukari karibu shilingi bilioni 700, barabara ya lami shilingi bilioni 150, mradi wa maji shilingi bilioni 41, umeme shilingi bilioni 24, tumejenga shule mpya, tumejenga vituo vya afya, kituo cha polisi na mambo kibao. Haya yote

yalikuwa ni changamoto, lakini katika mpango uliopita yametekelezwa na yamefanyika. Sasa anatokeaje mwanasiasa huko mzee mchekea mwezi analalamika lile Bunge mnaliona la kupongeza tu. Kinamkera nini sisi tukiendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zitaendelea kuwepo, tumesema mara kadhaa mpaka mwisho wa dunia, lakini sisi tunampongeza Mheshimiwa Rais wetu kumpa *comfort*, kumpa nguvu, kumpa moyo zaidi na wasaidizi wake katika kazi kubwa wanayoifanya katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu kidogo niseme changamoto; katika Jimbo letu la Kilombero tuna changamoto ambazo zimetokana na utekelezaji wa mpango wa mwaka jana. Kwa mfano, tumepata kiwanda kipya cha sukari chenye thamani karibu shilingi bilioni 700 na tunaishukuru Serikali, lakini wakulima sasa hivi wana-*experience* kuchelewa kulipwa na kupungua kwa bei ya sukari, tuna changamoto ya barabara zetu, tumepata mafuriko sisi na Rufiji kuliko mtu mwingine yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba katika utekelezaji wa mpango unaokuja mtatusaidia kata 19 za Ifakara bado zina mashimo na hali ni mbaya, tunaomba mitaro na tunaomba madaraja. Pale Chicago kwa mfano barabara katika Kata ya Kidatu hakuna, kivuko cha Kidatu A kwenda Kidatu Kati, Daraja la Msola stesheni kuunganisha na Kata ya Mang'ula limekatika kabisa. Mji wa Ifakara wenyewe sasa hivi una hali ngumu. Kwa hiyo, hiyo ni changamoto mojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo hilo la mafuriko na sisi tunajaza kwa 65% Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tunaiomba sana Serikali na tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ametusaidia tumeweza kujenga tuta upande mmoja basi tunaomba tupate na tuta upande wa pili ili tuweze kukamilisha maendeleo yetu ya jimbo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha upo hapo na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, mimi nataka kusema hili jambo ambalo lipo changamoto katika jimbo langu ili unisaidie na namshukuru sana Mheshimiwa Mkuu wangu wa Wilaya ameweza kulituliza jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliendа jimboni kwetu, ametuzindulia daraja kubwa la Kidatu ambalo zamani tulikuwa tunapishana kwa magari kwa kusubiriana, ametuzindulia barabara mpya yenye kilometa 67 haijapita mwezi. Hata hivyo, nataka kukwambia sasa hivi ninavyokwambia, mkandarasi yule ameondoa watumishi (vijana wetu wote kazini) na amefungia vifaa ndani kwa sababu hajalipwa na mkandarasi anaitwa *Reynolds Construction Company*. Amewapa likizo kila mara watumishi wale vijana wetu na tunaenda kwenye Serikali za Mitaa na wengine walikuwa wamekuja Dodoma hapa jana na juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nilikuwa nakusubiri sana nikwambie jambo hili. Nakuomba yule mkandarasi alipwe na *TRA* anayoidai ama na Serikali mumlipe ili matunda ya ile barabara katika utekelezaji wa mpango uliopita tuweze kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu mimi nizungumze kidogo kuhusu kipengele cha malengo mahsusi ya mapendekezo ya mpango. Kipengele cha sita kinasema; "Kuendeleza kuimarisha amani, utulivu wa kisiasa nchini pamoja na usalama wa Watanzania." Tunaweza tukaongea yote haya, lakini tunajifunza katika nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipolinda amani yetu katika nchi yetu utekelezaji wa mpango huu hatutoupata na tunajifunza katika nchi ya jirani. Ninaona kwenye mitandao, baadhi ya vijana wenzangu wanaona chokochoko kama Watanzania malofa kwa sababu hawaambukizwi na mambo yanayotokea katika nchi za jirani. Nawasihi vijana wenzangu, kuwaasa na kuwaomba tusikubali kusikiliza haya ya mzee mchekea mwezi, tulinde amani yetu kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu nizungumzie sasa vitu vitatu ama vinne kwa haraka haraka, kwanza nataka kuzungumzia *population*. Tunavyo-*calculate* maendeleo ya nchi yetu tuna-*calculate* mapato yetu yote kwa ujumla tunagawanya kwa Watanzania wote bila kujali nani anacho, nani hana na ndiyo tunapata *per capita* hiyo *development.* Mheshimiwa Waziri nawaomba sana, ni nani anafuatilia *population* ya nchi yetu?

Tunajua ongezeko la watu linaenda sawa sawa na mahitaji ya *labour force,* siyo? *Cheap labour* kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Mawaziri niwaambie, mimi nilienda Mwanza pale na Kamati, juzi tulikuwa Dar es Salam tunaangalia *TBC* inavyorusha watoto wa Taifa hili wanavyolala kwenye maduka usiku. Watoto wa Taifa hili pale Mwanza tumewakuta, mimi nimewahoji angalia ile *video* yangu, watoto hawawajui baba, mtoto hajui mama. Sasa kama tunataka kwenda kwenye maendeleo ya kweli na Mheshimiwa Msambatavangu alishawahi kusema hapa siku moja, lazima tujiulize kijana wa kike na wa kiume wakiamua katika starehe zao kuzaa, watawajibika kulea. Hakuna Taifa ambalo tunaweza tukatelekeza watoto barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa na Mheshimiwa tunatoka pale nje tumekuta mama amebeba watoto watatu, kila mtoto na baba yake na wanaume wote wamemkimbia yule mama. Mama yule siku akichoka akitelekeza wale watoto, wanahesabika ni maskini wa Watanzania. Waheshimiwa Mawaziri haikubaliki, taasisi zinazohusika tunaomba sana msimamie *population* yetu, mui-*control* vizuri ili iweze kwenda na maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *video* moja maarufu sana yule kijana wa Mbeya na mimi namtafuta, anayesimamisha vijana wenzake wa bodaboda anawaambia siyo ujanja kuzaa, kuzalisha wanawake na kupeleka kwa bibi. Anawaambia mimi nalea watoto wangu watatu nyumbani kwangu ni bodaboda, hata Mheshimiwa Hakimu akinihukumu leo anaweza kunipunguzia adhabu kwa sababu nalea mwenyewe. Kawakusanya vijana wenzake anawaambia wewe fulani huo ni ulofa, umezalisha watoto wanne umepeleka kwa bibi. Unazalisha unasema wanawake wanaojileta unazalisha tu. Watoto wanaenda mtaani, watoto yatima wanazidi na sasa hivi tuna utamaduni wa kujenga vituo vya watoto yatima, hatulei watoto yatima katika majumba yetu. Hatuwezi kufikia maendeleo ya kweli kama tunaongeza *population* ya namna hiyo ya holela holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nigusie *TRA;* yote haya ya mpango na utekelezaji yanataka mapato, tulisema katika Taarifa ya *PAC* hapa. *TRA* wanataka kuwezeshwa kuwekeza katika mifumo ili wawajue walipakodi wote katika nchi hii. Tunaomba sana mtusaidie, *TRA* iweze kupatiwa fedha hizo iweze kukusanya mapato, lakini vinginevyo hapa hatutaweza kukamilisha mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishoni nataka kumalizia kwa kusema mimi naunga mkono hoja. Nasisitiza sana ili tupate maendeleo lazima tuangalie kila Mtanzania, kila kijana wa Kitanzania anayezaliwa anamulikwa katika nchi hii. Akizaliwa tunampa cheti cha kuzaliwa kinakuwa na namba ambayo ndiyo *account* ya benki yake ya Taifa na ndiyo kitambulisho chake cha Taifa hili na wazazi wake wawajibike kumtazama mtoto yule mpaka anapopata elimu ya msingi na elimu ya ufundi. Vinginevyo hatutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari, ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai, lakini nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nitoe mchango wangu kwenye Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri wao na watendaji wao wote kwa kuleta mpango huu mzuri. Mpango huu una mambo mengi mazuri na kwa sababu hiyo tuna kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kama msimamizi na kiongozi katika utekelezaji wa mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ambao una dhamira ya kujenga uchumi jumuishi, kupunguza umaskini, kuzalisha ajira na kuongeza mauzo ya bidhaa za nje. Kwenye hili la mauzo ya

bidhaa za nje ukiona taarifa ya mpango ilivyowasilishwa inaonesha mauzo ya nje tumeuza chini ya kile ambacho tumenunua na kwa maana hiyo tuna urari hasi. Kwa namna yoyote ile katika mpango unaokuja ni lazima tuendelee kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji ili kuendelea kujenga msingi wa uchumi jumuishi, kupunguza umaskini na kuzalisha ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili hakuna namna yoyote tutakwepa kuimarisha na kuendelea kuwekeza kwenye Sekta ya Kilimo. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Bajeti inaonesha kwamba Taifa letu lina watu takribani milioni 28 wanaohusika moja kwa moja na kilimo ambao ni karibu zaidi ya 40% wananchi tulionao. Kwa hiyo, hakuna namna yoyote ile tutakwepa kuwekeza kwenye kilimo, kuendelea kuwekeza kwa nguvu kubwa. Kwa maana hiyo nitaongelea kwenye eneo hili la kilimo, lakini nitaongelea vilevile kwenye uhifadhi wa mazingira nikihusianisha na uwekezaji kwenye nishati ya umeme, lakini pamoja na miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna kilometa za mraba takribani 945,000. Katika eneo lote hili karibu kilometa za mraba 61,500 ni eneo la maji na katika eneo hili tuna hekta karibu milioni 29.4 ambazo tunaweza tukazitumia kwa kilimo. Tafsiri yake ni nini? Tukiendelea kuwekeza kwenye kilimo yote haya kama kipaumbele tunaweza tukayafikia, kupunguza umaskini, kutengeneza ajira na kutengeneza uchumi jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia malengo waliyonayo Wizara ya Kilimo, kwa mfano, mpango wa mwaka jana, walipanga mpaka kufikia mwaka 2025 angalau kilimo cha umwagiliaji tuwe tumefikia hekta milioni moja, lakini hivi tunavyoongea bado tuko kwenye hekta laki saba pekee jambo ambalo linaonesha kwamba tunahitaji kuendelea kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji, lakini siyo kuwekeza tu kwenye kilimo cha umwagiliaji, tuwekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji chenye tija, ndiyo maana jana, Mheshimiwa Mwijage alichangia hapa, tunapaswa kuangalia maeneo yenye rasilimali tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa tunawekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji, lakini kuna maeneo ambayo yana rasilimali maji, ni namna gani tumetumia rasilimali hizi. Nimelisema hili takribani kila mwaka, lakini tuna kila sababu ya kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji tukitumia rasilimali tulizonazo. Tufanye kilimo cha umwagiliaji, lakini kilimo cha umwagiliaji chenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wananchi wetu wanafanya kilimo cha jembe la mkono, uwekezaji unaotakiwa ni kuwatoa kwenye kilimo cha jembe la mkono ili wafanye kilimo chenye tija. Wenzetu pale Misri wanategemea maji kutoka Ziwa Victoria kupitia Mto Nile, kule ni jangwa, lakini wanazalisha mazao wanalisha nchi karibu 17 kwa kilimo chenye tija, kilimo cha umwagiliaji na sisi twende kwa mfumo huo ili tuweze kukabiliana na changamoto tulizonazo za ajira na kujenga uchumi jumuishi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kama Ukerewe, tuna kilometa za mraba 6,400 ni 10% pekee ndiyo ardhi, lakini tuna hekta karibu 4,000 zinazoweza kufanyika kilimo cha umwagiliaji. Ninashukuru kwamba Wizara ya Kilimo kuna jitihada inafanya, lakini ni vizuri rasilimali kama hizi tukazitumia kwa tija ili kupunguza changamoto tulizonazo kama ilivyo Ukerewe na maeneo mengine ambayo yana rasilimali maji kama ilivyo kwenye hilo eneo. *(Makofi)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa, Kunambi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, umehama sehemu yako.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahishwa sana na mchango wa Mheshimiwa Mbunge

anayechangia sasa. Kimsingi ukisoma historia ya maendeleo yaliyofanyika huko Ulaya, karne ya 16 wenzetu walianza na mapinduzi ya kilimo baadaye wakaenda kwenye teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mchango wake ni mchango mzuri sana na ametaja maeneo ambayo kimsingi ukiwekeza kwenye umwagiliaji huna sababu ya kuweka fedha nyingi. Maeneo hayo ni pamoja na Morogoro, Mkoa wa Morogoro…

**MWENYEKITI:** Malizia Taarifa yako, maana unachangia sasa, mpe Taarifa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamueleza tu, ninasema maeneo kama Morogoro kuna mito ya kutosha, kimsingi ukiwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji, huna sababu ya kuweka fedha nyingi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkundi, unaipokea taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Kunambi?

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu sana kuwekeza, jana nilimsikiliza Mheshimiwa Profesa Manya akichangia juu ya umuhimu wa kuwekeza kwenye gesi na alitoa mawazo na ufafanuzi mpana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwekeza kwenye sekta ya kilimo, lakini tuhakikishe sekta ya nishati, uwekezaji wake unakuwa mkubwa na nishati inawafikia wananchi kwenye Taifa hili. Nipongeze Serikali, tumejenga vyuo vingi vya ufundi kupitia *VETA*, tuna shule za sekondari, masomo ya sayansi watoto wanasoma, lakini bila nishati ya umeme haya yote tunayoyafanya bado tutaendelea kwenda kwa kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali, katika vijiji zaidi ya 64,000 tuna vijiji karibu 36,000 ambavyo tayari vina nishati

ya umeme, lakini tuna vitongoji vingi bado havina nishati hii ya umeme. Ninashauri ili twende vizuri zaidi, ni vizuri sana tukafanya tathmini kwa kuangalia kaya zenye nishati hii ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa pendekezo langu ninashauri, sioni tija sana kwamba maeneo yaliyoko mjini yalipe umeme shilingi 300,000 kupata nishati hii ya umeme, maeneo ya vijijini walipe shilingi 27,000, tungeweka kiwango sawa. Pendekezo langu ninashauri, ikiwezekana wananchi wapewe umeme bure halafu wanapokuwa wanalipa *bill* ndiyo wawe wanakatwa kiasi fulani ili kufidia gharama iliyotumika kupeleka umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili litaongeza tija kwenye uzalishaji, litaongeza tija kwenye ubunifu na watu wetu watatumia nishati ile kujiletea maendeleo na kujenga uchumi kwenye Taifa hili ikiwa ni pamoja na kuongeza walipa kodi kwenye Taifa hili na kupandisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mkundi, sasa nimwite Mheshimiwa Sichalwe, anafuatia na Mheshimiwa Masache Kasaka, Mheshimiwa Robert Chacha Maboto ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi na ninaunga mkono hoja zote ambazo zimewasilishwa hapo mezani na mchango wangu utajielekeza kwenye vyanzo vya mapato na nimeweka katika makundi manne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha kwanza cha mapato; kabla sijaanza kuelezea chanzo hicho cha mapato, ninaomba ni-*quote* kitabu kitakatifu Biblia kwenye mistari kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisome Kutoka 4:1-8 nao unasema; "Musa akajibu akasema, lakini, tazama, hawataniamini, wala hawataisikia sauti yangu; maana watasema, BWANA hakukutokea. BWANA akamwambia, ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? Akasema, Ni fimbo. Akamwambia, itupe chini;

akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake. BWANA akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, ukamshike mkia; (akaunyosha mkono wake akamshika mkia, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake); ili kwamba wapate kusadiki ya kwamba, BWANA Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amekutokea. BWANA akamwambia tena, Sasa tia mkono wako kifuani mwako. Akautia mkono wake kifuani mwake; naye alipoutoa, kumbe! mkono wake ulikuwa una ukoma, ghafla umekuwa mweupe kama theluji. Akasema, Tia mkono wako kifuani mwako tena. Akautia mkono wake kifuani mwake tena, na alipoutoa kifuani mwake, kumbe! umerudia hali ya mwili wake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mstari wa nane na wa mwisho; "Basi itakuwa, wasipokusadiki, wala kuisikiliza sauti ya ishara ya kwanza, wataisikiliza sauti ya ishara ya pili."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma tena Kitabu hicho hicho cha Kutoka 17:4–6, maandiko yanasema; "Musa akamwambia Bwana, akisema, niwatendee nini watu hawa? Bado kidogo nao watanipiga kwa mawe. Bwana akamwambia Musa, pita mbele ya watu, ukawachukue baadhi ya wazee wa Israeli pamoja nawe; na ile fimbo yako ambayo uliupiga mto kwayo, uitwae mkononi mwako, ukaende. Tazama, nitasimama mbele yako huko, juu ya lile jabali katika Horebu; nawe utalipiga jabali, na maji yatatoka, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli. Ameen." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema nini, lengo la maandiko haya, fimbo hiyo hiyo ambayo nimesoma katika sura hizi mbili tofauti ndiyo fimbo hiyo hiyo wana wa Israel waliitumia Musa akapiga mto, mto ukagawanyika wakapita katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha kwanza cha mapato; chanzo cha kwanza cha mapato ni mapato yetu ambayo yako tayari yanajulikana kwenye vyanzo vyetu vya mapato vilivyopo. Changamoto iliyopo ni namna ambavyo hatuzitendei haki taarifa za *CAG*. Mapato tuliyonayo tungeamua kuzitendea kazi zile taarifa za *CAG*, vyanzo vilevile tulivyonavyo vingeweza kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukulia hii ni kama fimbo ya Musa kwamba kile tulichonacho tukiamua kuking'ang'ania na kukitumia vizuri kinaweza kufanya maajabu na kutenda maajabu ndani ya Taifa letu, lakini kwa sababu imani yetu imepungua hata ambapo Waheshimiwa Wabunge tukiongea hatusikilizwi, *CAG* akileta taarifa hapa Bungeni akisoma, mtu anakuja kujitetea mbona *CAG* ametupa hati safi. *CAG* ametoa hati safi wakati kule ndani ameeleza kuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tayari sisi tunayo fimbo ambayo ingeweza kufanya mambo makubwa ingeweza kupasua mto katikati na tukapita. Kwa hiyo, tunapotafuta vyanzo vipya vya mapato, kwanza tuangalie mkononi kwetu tuna nini, kwenye mkono tunayo fimbo ambayo inaweza ikageuka ikawa nyoka na bado tukaitumia ikaweza kutuletea maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vyetu hivi vya mapato tuvitendee vizuri na tusione Taarifa ya *CAG* kama ni kwa ajili ya kutukosoa, Taarifa ya *CAG* ni kwa ajili ya kutuimarisha. *CAG* mlinzi kwenye nyumba yetu ambaye tumemuweka analinda vitu vyetu vya thamani, lakini mlinzi huyo anapokwambia nimeona changamoto, tena unamwambia hakuna shida, huyo mwizi anayetaka kuiba wewe muache tu. Sasa ulimuweka wa nini? Si ulimuweka aweze kukulindia mali zako za thamani, anakusaidia kujua hapa pana shida, hapa pana shida, ungechukua taarifa yake ukaifanyia kazi vizuri inawezekana usingeweza kupata shida. Kwa hiyo, vyanzo vyetu vya mapato tulivyonavyo sasa, tuweze kuvilinda na tutumie Taarifa za *CAG* ili tusiendelee kutoboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha pili ni biashara za *cross borders, international trade;* biashara nyingi ambazo ni *international trade* hakuna mahali ambapo hazifanyi vizuri. Tumeshuhudia namna ambavyo zinafanya vizuri, nami sitaacha kuongelea soko la *DRC*. Soko la *DRC* sisi tuko hapa tumepakana na Congo uso kwa uso, lakini mataifa yanayotoka mbali yananufaika na Congo vizuri. Hatutumiii neema ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu, na yenyewe hii ni fimbo nyingine Mungu ametupa, tungeweza kuitumia vizuri, ingeweza kuleta miujiza na matokeo mazuri kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Oktoba, 2024 wiki moja tu ambayo imepita Serikali ya China pamoja na Serikali ya *DRC* ilizindua barabara yake yenye urefu wa kilometa 466 kutoka mji wa Kalemii, Jimbo la Tanganyika kwenda Manono ambako China wamejenga kiwanda kikubwa sana cha kuzalisha *lithium* na wanatarajia kusafirisha hiyo *lithium, metric* tani zaidi ya laki tano kutoka Bandari ya Kalemii kuja kwenye Bandari yetu ya Kigoma, watatumia *railway* tunaita *SGR* kwenda kutumia *Dar es Salaam Port* na kupeleka China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara kadhaa nimekuwa ninaongea hapa kwamba kwa nini na sisi tusijenge barabara kutoka Kalemii au Moba kuelekea Lubumbashi ambako kuna soko? Lakini Mchina huyo huyo ameshaanza kujenga *railway* kutoka Angola kuja Lubumbashi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa China anakotoka huko Bara la Asia kuja mpaka huku kwetu na sisi *DRC* tunaye hapa, basi wazo langu maadamu Mchina ameshaweka barabara kutoka Manono kuja Kalemii, Jimbo la Tanganyika *DRC*, na sisi tuka-*connect* barabara kutoka Manono kwenda Lubumbashi ambazo zinapungua zinakuwa kama kilometa 470 hivi wakati tunaendelea kujenga barabara kutoka Moba kwenda Lubumbashi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yote ni kwa faida gani? Ni kwa faida yetu wenyewe. *I don't think* kama China kusingekuwa na manufaa ya mambo yote haya angeamua kuweka uwekezaji wote, *as we are speaking now* ukiangalia nchi ambayo inaongoza kufanya biashara na *DRC,* sisi hata kwenye *top four* hatupo na ni majirani zetu. Kenya wapo huko mbali wanafanya vizuri biashara na *DRC*. Soko la Congo siyo la kupuuza litaleta ajira nyingi sana kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kingine cha tatu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitimisha.

**MWENYEKITI:** Lakini hitimisha.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha tatu cha mapato ni *border;* nimeshachangia tena hapa kwamba pale Momba tunalo *gate* ambalo katika kutoa michango yetu, wenzetu upande wa pili Zambia walivyogundua wameshaweka *gate toll.* Kwa hiyo, chochote kinachopita kule kwao kinapita wanaingiza mapato, lakini sisi kwetu magendo yanaendelea kuingia, yanaendelea kupita, njia iko wazi, kwa hiyo, ni jambo la muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tuwekeze kwa wakulima, mkulima wa nchi hii bado analima kwa kutumia jembe la mkono. Tuwekeze kwa mkulima kwa sababu ndiyo chanzo kimojawapo cha mapato ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa tunaomba Vodacom wapunguze gharama za ma-*bundle*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester Sichalwe kwa mchango wako.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, anafuatiwa na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninashukuru kwa kupata nafasi niweze kuchangia kwenye mpango huu ambao uko mbele yetu na nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya na kuhakikisha mpango huu unaenda kumkomboa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo imeeleza kwenye kauli yao kwamba mpango wa maendeleo unalenga kuboresha hali ya maisha ya Watanzania na kujenga uchumi imara na shindani na sisi tunataka tuone mpango huu namna ambavyo

unaenda kuboresha maisha ya Watanzania, lakini vilevile kuendelea kuboresha uchumi wetu uendelee kuwa imara na ushindani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mipango ya Serikali imekuwa inapangwa kila mwaka na ile ya miaka mitano, na ile ya miaka 25. Ni mipango mizuri na ambayo utekelezaji wake tunakuwa tumeuona, sisi sote humu na Watanzania wote wamekuwa mashuhuda namna ambavyo miradi mingi na ya kimkakati ambavyo imefanyika ndani ya nchi yetu. Ninaipongeza Serikali, nampongeza Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba hakuna kilichosimama, mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango hii mizuri ambayo ipo kwenye huu mpango wetu, lakini ili utekelezaji wake uweze kwenda vizuri kuna baadhi ya maeneo ya kuweza kushauri ili yaweze kukaa vizuri na utekelezaji wake kweli uweze kumnufaisha huyu Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku juu Tume ya Mipango pamoja na Wizara zinapanga vizuri na upangaji huu upo kwenye *level* ya huku juu ya Wizara, lakini tunaposhuka huku chini bado kuna changamoto ya hizi taasisi zetu kuweza kuongea lugha moja na kuweza kusomana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, leo kuna barabara zinajengwa na *TARURA,* barabara za lami au za changarawe, lakini mahali ambapo barabara hizi zinapita, ipo miundombinu mingine ambayo inapita, ipo miundombinu ya maji, umeme na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watu wa *TARURA* wanapotengeneza hizi barabara unakuta hawahusishi watu wa maji na matokeo yake wanaharibu miundombinu ya maji pamoja na miundombinu mingine ilhali hawa watu wa maji na miundombinu mingine hawana bajeti ya kuweza kurekebisha hii miundombinu. Matokeo yake, leo barabara zinatengenezwa vizuri, lakini tunaenda kutengeneza changamoto nyingine ya maji na miundombinu baadhi ya maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe na nishauri, mipango ambayo inapangwa kuanzia ngazi ya huku juu Wizarani mpaka chini kwenye Serikali za Mitaa tuone namna bora ya kushirikisha hizi taasisi ili tusiwe tunafanya kazi ya kurudia rudia na kuingia gharama mara mbili. Niombe sana mlichukue hili na muweze kwenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimeona kwenye mpango hapa wameeleza namna ambavyo Serikali imepanga kutumia zaidi ya shilingi trilioni 16 katika mipango mbalimbali na miradi ya maendeleo. Ni fedha nyingi, lakini kwa namna ambavyo miradi ya nchi hii inavyokwenda bado fedha hizi ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali pamoja na kwamba tunategemea kodi kuweza kupata hizi fedha, misaada pamoja na mikopo mbalimbali, tuone namna ya kuongeza walipa kodi wengine ili fedha hizi ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *TRA* pamoja na Serikali bado tunaendelea kuwakamua walipa kodi walewale Watanzania. Tunazibadilisha kodi kwa majina tofauti, lakini bado walipa kodi ni walewale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali ione namna bora ya kuboresha mazingira ili tuweze kuwatengeneza wafanyabiashara wapya ili waweze kulipa kodi mpya na ili tuweze kuongeza mapato kwenye nchi yetu, hii ndiyo itakuwa namna bora na nzuri ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili yake, tuna wafanyabiashara mitaji yao ni midogo, Serikali itumie hii nafasi ya kuona namna nzuri ya kuweza kuwasaidia kuweza kuwainua wao ili tuwatengeneze wafanyabiashara wakubwa pamoja na mabilionea wapya kwenye nchi yetu hii ya Tanzania. Hii itaweza kutusaidia kuboresha mazingira mazuri ya biashara ili wafanyabiashara wetu hawa waweze kufanya biashara katika hali nzuri zaidi, lakini tukiweza kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la nishati; kila mmoja hapa ameweza kuzungumza namna ambavyo Serikali yetu imeweza kupambana kuhakikisha Bwawa letu la Mwalimu Nyerere limeweza kukamilika na sasa hivi tuna nishati ya uhakika ya umeme tunao wa kutosha, hii tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo na kuwa na umeme wa uhakika, Serikali sasa iwekeze nguvu kwenda kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa huu umeme. Bado kuna baadhi ya maeneo mengi umeme unakatikakatika, lakini ukiuliza, changamoto ni miundombinu ya umeme ambayo imeshachoka na imeshakuwa dhaifu. Hivyo, Serikali iweze kutumia muda huu kuweza kuboresha hiyo miundombinu ili umeme uweze kupatikana wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, (b) yake; baadhi ya maeneo tunapata umeme mdogo. Nami kule kwangu baadhi ya maeneo, Chunya, Makongorosi na maeneo ya Tarafa ya Kipembawe, umeme umefika, lakini umeme ni mdogo. Hivyo, bado wananchi wanashindwa kunufaika na ule umeme ambao unakuwa umefika kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali, ni muda mwafaka wa kujenga *substation* ili kuweze kupata umeme wa uhakika, wenye nguvu ili wananchi hawa waweze kunufaika na umeme wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, (c) yake; pamoja na kwamba umeme ni huduma Serikali inapeleka, pia umeme ni biashara, pamoja na kwamba umeme ni biashara sasa tutumie nafasi hii kuweza kupeleka umeme kule kwenye uhitaji mkubwa ili wananchi wa Tanzania waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaotoka kule Chunya ambako tuna wachimbaji wengi wadogo wadogo, wana uhitaji mkubwa sana wa umeme. Hivyo, Serikali iweze kuona na kuwekeza nguvu za kutosha ili kuhakikisha kwamba umeme huu unawafikia wachimbaji wengi kwenye maeneo yao ili waweze kuutumia,

kuzalisha vya kutosha na waweze kuununua kwa sababu hii ni biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niweze kutoa ushauri, kama bado Serikali inaona kwamba kupeleka umeme kule gharama ni kubwa, iwakopeshe hawa wachimbaji wetu wadogo wadogo ili wanapokuwa wananunua umeme wawe wanalipa kidogo kidogo na ndiyo tutaweza kuwasaidia hawa wachimbaji wetu na wengi wataweza kufikiwa na umeme huo na itaweza kuwasaidia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo limeelezwa kwenye Mpango ni sekta ya madini. Niishukuru Serikali, sekta ya madini imeweza kufanya kazi vizuri, lakini pia Serikali imeweza kwenda kuboresha mazingira ya madini. Leo imeweza kufikia zaidi ya 9% kwenye mchango wa Pato la Serikali, hii ni hatua kubwa sana. Hata hivyo, pamoja na haya 40% ya pato hilo bado ni kutoka kwa wachimbaji wadogo ili tuweze kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo hawa tunawawekea mazingira mazuri ili waendelee kuzalisha vizuri zaidi. Kubwa zaidi, tuendelee kuwekeza kwenye tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuwekeza kwenye utafiti kwa wachimbaji wadogo, wataweza kuchimba uchimbaji wao mzuri zaidi na watazalisha vizuri zaidi. Pia tutaweza kupata kipato kikubwa na ile 11% ambayo Serikali iliweza kuipanga, tutaweza kuifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, naunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasaka, ahsante sana kwa mchango wako. Nimwite sasa Mheshimiwa Robert Maboto, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, ajiandae.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Awali ya yote ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye

Mpango wa Serikali wa mwaka 2025/2026. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ambayo leo nimeipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye Jimbo langu la Bunda Mjini ambapo zaidi ya miaka 30 iliyopita wananchi wangu wa Kata ya Nyatwali wamekuwa wakiishi katika maisha ambayo walikuwa hawawezi kujua mwanzo wao na mwisho wao. Hata hivyo, changamoto hiyo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameitatua kwa sababu hawa wananchi muda wote wameambiwa kwamba maeneo yale wanayoishi wangetakiwa kuhama. Kwa hiyo, zaidi ya miaka 30 iliyopita walikuwa hawawezi kujifanyia maendeleo yao ya msingi kwa sababu wana mambo mawili, ama wanaweza kuondoka kwenye eneo hili, ama inawezekana wakaendelea kuishi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo hili lilikuwa linawaletea watu umaskini mkubwa kwa sababu walikuwa hawawezi kupanga mipango yao ya miaka ijayo, kwa sababu wanahisi tu muda wowote kwa chochote watakachokifanya pale wanaweza kuondolewa. Hata hivyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake, imelipa zaidi ya shilingi bilioni 60 kwenye Kata ile ya Nyatwali na kuwafanya wale wananchi wetu waweze kwenda kupata mahali pao papya pa maisha yao mazuri ambayo na wao itawafanya wafanye mipango yao endelevu kwa ajili ya wao wenyewe na vizazi vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilikuwa ni kero kubwa katika Jimbo la Halmashauri ya Bunda Mjini. Kwa hiyo, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi hii kubwa aliyoifanya, lakini pia ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo alitupatia msaada mkubwa kwenye jambo hili ili kuhakikisha kwamba jambo hili linafikia mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru pia Waziri wa Fedha, Mkuu wangu wa Mkoa wa Mara pamoja na Mkuu wa

Wilaya ya Bunda kwa namna ambavyo tumeshirikiana kwenye jambo hili. Wananchi wetu wale wameishi katika kadhia kubwa kwa muda mrefu. Hawawezi kuvuna, kujenga wala kufanya chochote kwa sababu tu wanaambiwa kwamba muda wowote wanaweza kuhama. Sasa kwa sababu Serikali imetatua tatizo hili, imewafanya wananchi wetu waweze kupata mwelekeo mpya na mpango mpya wa maisha yao huko wanakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninasema ahsante sana kwa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi hiyo kubwa ambayo wameifanya kwa ajili ya wale wananchi wetu wa Jimbo la Bunda Mjini hasa ile Kata ya Nyatwali, kwa kuwafanya sasa na wao waweze kupanga mipango yao mizuri katika maisha yao. Pia ninaamini huko ambako wao wamekwenda, watakwenda kufanya vizuri kwa sababu Serikali imewalipa fedha zao vizuri, ingawa bado kuna changamoto ndogo ndogo ambazo ninaamini tu kwamba bado Serikali inazishughulikia na itazitatua changamoto hizo zikaisha vizuri, ili wale wananchi wetu waweze kuishi vizuri katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika Mpango huu, ni kuiomba Serikali kuhakikisha kwamba Mpango huu unachukua jambo kubwa ambalo wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini wanalitegemea. Kumekuwepo na ule Mradi wa *TACTIC* ambao kwa muda mrefu wananchi wetu wameahidiwa na bado jambo hili halijafanyiwa kazi. Pia ndilo deni kubwa ambalo limebaki katika Halmashauri ya Mji wa Bunda. Niombe katika mipango hii, jambo hili nalo liingizwe ndani ili utekelezaji utakapoanza mradi huu uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la maji; mpango huu ujikite pia katika kutatua changamoto za maji kwa wananchi wetu. Huko tunakokwenda maeneo yanazidi kuongezeka, idadi ya Watanzania inazidi kuongezeka. Kwa hiyo, tatizo la maji bado litaendelea kuwepo. Kwa hiyo, lazima mpango useme kwa muda mrefu kuwa tatizo la maji litatatuliwa vipi kwa wananchi wetu, kwa sababu kila leo tunapokamilisha na kusema mfumo wa maji umefikia hapa na wananchi walikuwa wanaishia hapa, baada ya mwaka mmoja wananchi

wameongezeka na eneo limepanuka zaidi. Kwa hiyo, tatizo la maji linazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la umeme, kwa sababu Serikali yetu imekamilisha Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo linatusambazia umeme kwenye nchi yetu, kwa sasa Serikali inakwenda kusambaza umeme kwenye vitongoji, na vitongoji ndiyo mahali pa mwisho ambapo wananchi wetu wanaishi hasa wale ambao ni wakulima na wafugaji ambao pia siyo wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilidhani mpango pia ungesema kwamba hawa wananchi badala ya kuwaambia watoe fedha za kuunganishiwa kwenye umeme, wao waruhusiwe na Serikali iwaunganishie umeme kwenye maeneo yao. Baada ya kuwaunganishia umeme, hawa wananchi walipe ile gharama ya kuunganishiwa umeme kupitia bili zao. Kwa nini? Kwa sababu hawa ni wakulima, wafugaji na ni wale watu ambao wanaishi katika hali ya maisha ya chini kabisa. Pia kwa sababu sasa hivi umeme katika nchi yetu unazalishwa kwa kiasi kikubwa, mimi ninadhani Serikali itengeneze mpango wa kwamba hawa wananchi na wao waunganishiwe umeme ili na wao wanufaike na jambo la umeme kama vile Watanzania wengine wanavyonufaika na umeme. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maboto, kengele ya pili, ninaomba unga mkono hoja.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nimwite sasa Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, atafuatiwa na Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu wa Maendeleo kwa ajili ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wa Maendeleo nilikuwa ninaangalia katika eneo ambalo linanigusa, naona ni namba 2, 3 na 6 kitu kama hicho. Hili eneo lilikuwa linazungumzia maisha ya watu na hali ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikiri kwamba Mheshimiwa Profesa Mkumbo ni mwalimu wangu, kwa hiyo, pamoja na kuandaa kilichoandaliwa na mwalimu wako na hasa alinifundisha katika eneo hilo hilo la watu, umaskini, pamoja na siasa na namna ya kuwaondoa watu katika umaskini. Hili somo ni kwamba Profesa alinifundisha na mimi ninalifanyia kazi. Sasa siwezi ku-*doubt* chochote hapo kuhusiana na mwalimu, ila ninataka kumkumbusha tu mwalimu wangu kwamba katika hili kuna maeneo ambayo ameyasahau hasa ya wananchi maskini walioko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kutengeneza furaha ya wananchi wa Tanzania, ni kwamba lazima uwaangalie wananchi maskini walioko vijijini, hali zao na watatoka vipi katika zile hali. Kwa hiyo, katika mpango wako na katika jambo hili, kule vijijini maisha ni magumu sana na ni maisha yao ya kila siku. Mheshimiwa Profesa pamoja na Waziri wa Fedha, bahati nzuri ninyi nyote ni watoto wa maskini, mmefika katika hatua hii, mnajua kilichoko kule kijijini hususani katika Jimbo la Iramba mnajua kabisa kwamba magulio ni sehemu ya maisha ya wananchi kwa kila siku. Liangalieni Gulio la Shelui na Ndago, haya ni magulio tu ambayo nawapeni mfano wake yalivyo, lakini angalie Gulio la Kinampanda wananchi wanategemea kuendesha maisha yao na kuhudumia familia zao kutokana na gulio. Kwa hiyo, gulioni wanakwenda kuuza na kununua vyakula vya kutumia. Watatunza vyakula vyao mpaka gulio lingine tena labda Jumamosi au Ijumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Mpango wenu wa Maendeleo, sijaona kabisa kwamba hawa wananchi wa namna hiyo mnawasaidia kwa namna gani, kwa sababu kule ndiko ziliko biashara ndogo ndogo zinazowafanya wananchi sasa waweze kutoka katika umaskini na wanapata pato lao la wiki na pato la mwezi linategemea kutokana na magulio. Hali ya magulio nchini siyo nzuri. Magulio yetu hayana vyoo, hayana mabanda ya

kujikinga na mvua pale mvua zinaponyesha wakati watu wanafanya biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya magulio kuna minada. Iko minada mikubwa kwenye nchi hii, ukitembea kila mkoa na kila wilaya minada hii ipo. Hata hivyo, kwenye hiyo minada na yenyewe haijawekwa kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mizani; Waziri, Mheshimiwa Ulega alituahidi hapa kwamba atagawa mizani katika halmashauri ili iweze kuwekwa katika minada yetu. Watu wanafuga ng'ombe wao na mbuzi wao, wanakaa nao kwa muda mrefu (miaka mitatu), lakini anakwenda sokoni, anakwenda kupunjwa. Bei ya nyama sasa hivi zinaanzia shilingi 10,000, lakini mfugaji amekaa na ng'ombe wake anakwenda kumuuza kwa gharama ya chini. Hata hivyo, mizani ikiwepo, anaweza kumpitisha kwenye mizani na akajua hali aliyonayo. Hili halijawekwa kwenye Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakuomba sana Profesa hili jambo utusaidie sana kuliingiza ili kuangalia magulio yetu na wananchi watapataje mitaji ili kuweza kujiondoa katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la umeme, kwa mfano sisi pale Sengerema tunapokea umeme kutoka Mpomvu – Geita na tunapokea umeme kutoka Nyakato - Mwanza. Wakati tunatengeneza lile daraja (walipokuwa wanafanya upembuzi na usanifu), wakati wanafanya kazi ya kuchoronga kuangalia miamba chini, walikata ule waya na bahati nzuri wakati ule Waziri wa Nishati alikuwepo hapa Mheshimiwa January Makamba, alituahidi kabisa kwamba baada ya daraja kukamilika watapitisha waya darajani. Hili jambo halijafanyika na Mungu akijalia mwaka kesho daraja linafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba katika mpango tujue ile *cable* itarudishwa au haitarudishwi ili wananchi wa Sengerema sasa tujue nini cha kufanya kwa sababu Sengerema tuna tatizo la umeme kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la leseni ya mgodi wetu sisi, (Leseni ya Mgodi wa Nyanzaga). Mheshimiwa Profesa tulikwenda na wewe mpaka pale Nyanzaga, tumekwenda Nyanzaga kwa wale wamiliki wa awali wa mgodi ule wa *Sotta Mining,* tumepiga mikutano tuko na wewe na tumetembelea ile milima yote. Pia wakati wanakusomea taarifa walisema kwamba watapunguza kwenye leseni zao shilingi 225 na watatoa leseni 50 kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo kwa Wilaya ya Sengerema na Mkoa wa Mwanza. Lile jambo mpaka sasa hivi hawajafanya na mwaka 2025 Mungu akijalia wanaanza kujenga mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka kujua kwamba leseni hizo zitatolewa? Kwa sababu ilikuwa ni ahadi za mkutano wa hadhara na juzi amekuja kule Mheshimiwa Mavunde, amekuja kuwauliza na wao wakasema kwamba wao hawakutamka maneno hayo. Wewe ulikuwa ni Waziri wa Uwekezaji na uko hapa, tayari kuna mgogoro mwingine Sengerema wa kimaslahi kwa sababu tumesema hali ya umaskini na watu, hatuwezi kuwa na mgodi wananchi wanakaa wanauangalia. Pia mmeona migodi mingine yote (Nyamongo na wapi) mnaona fujo zinazotokea katika migodi. Sasa hili jambo tunaomba sana katika mpango wenu mliweke mara moja ili tuweze kuondokana na hali hii ya umaskini na kuwaondoa wananchi wetu wa Wilaya ya Sengerema katika hali ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni miradi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie hapo kidogo tu.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni wakandarasi wetu wa ndani, tunaomba wakandarasi wa ndani wawepo katika mpango wa kulipwa madeni yao.

Tunao makandarasi hali zao ni mbaya, wakandarasi wanauziwa nyumba zao na hivi tunavyozungumza wazabuni hali zao ni mbaya. Tunaomba kwenye mpango tuone tunawasaida kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam. Sasa ninamwita Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka na mwisho kabisa tutakuwa na Mheshimiwa Mohamed Issa.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu. Vilevile nitoe pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri wote wawili (Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Uwekezaji) kwa kutuletea mapendekezo mazuri na mwongozo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa moyo wake wa dhati kwa kuamua kuendeleza miradi iliyokuwa imeachwa na mtangulizi wake, mpaka sasa tija inaonekana na miradi inaendelea kuonekana. Kwa mfano ujenzi wa Daraja la juu la Kigongo – Busisi, ambalo utekelezaji wake umefikia 93%, daraja hili gharama zake zote kwa 100% zinagharamiwa na fedha za mapato ya ndani. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa dhati ya moyo wake kwa maamuzi haya makubwa kwa kuhakikisha daraja hili linakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa daraja hili italeta tija na kuchochea uchumi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Pia nami nishauri katika mpango huu ili hili daraja liweze kuleta tija zaidi, tujenge upya barabara ya kutoka Kisesa – Daraja la Simiyu – Bunda mpaka *Mara Border* Ili kuweza kufungua mipaka kwa ajili ya ufanyaji biashara katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa

maamuzi yake ya dhati ya kuwa na mikakati ya kukuza sekta ya uvuvi ili kuanza kunufaika na rasilimali zilizopo katika bahari kuu na kuchochea ukuaji wa uchumi wa bluu. Huu ni ujenzi wa bandari ya uvuvi pamoja na ununuzi wa meli ya uvuvi. Utekelezaji wa ujenzi wa bandari ya uvuvi umefikia 70%, ili ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, sekta ya uvuvi nchini ilikuwa bado haijaweza kunufaisha Taifa pamoja na kuwa na rasilimali za maziwa makuu, ukanda mrefu wa pwani, pamoja na bahari kuu. Kwa mfano, nchi ya Kenya yenye ukanda wa pwani wa kilometa 600 ilikuwa inachangia Pato la Taifa kwa 0.6%, lakini nchi yetu ya Tanzania yenye ukanda wa pwani kilometa 1,424 inachangia 0.03%. Mchango huu ni chini ya malengo ya mpango ambapo ilitakiwa kuchangia 1.9% ifikapo mwaka 2025/2026. Hivyo basi, naungana na ushauri wa Kamati kwamba ujenzi wa bandari ya uvuvi uende sambamba na kuweka mazingira ya biashara nyingine zinazoendana na bandari ya uvuvi, kwa mfano maeneo ya kuchagulia samaki *(sorting)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ilikuwa inafanyika nje ya nchi kwa kuwa Tanzania hatukuwa na bandari ya uvuvi wala miundombinu hii haikuwepo. Kwa hiyo, meli za nchi za nje zilizokuwa zinafanya uvuvi katika bahari kuu uchambuzi ulikuwa unaenda kufanyika nje ya nchi, kwa mfano nchi ya Shelisheli na hii ilikuwa inaikosesha nchi, ama kutokuwa na takwimu za uhakika kwa mfano, kwenye tozo ya *loyalty. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuwa na takwimu za uhakika kwenye ushuru wa *loyalty,* lakini pia samaki ambao walikuwa wanavuliwa nje ya mkataba, nje ya makubaliano, mapato yake yalikuwa hayafahamiki. Kwa hiyo, kama tutakuwa na miundombinu katika bandari yetu inayojengwa tutaweza kuokoa mapato yetu yaliyokuwa yanapotea kutokana na uvuvi na kufahamu *loyalty* ambayo tunatakiwa tuipate katika uvuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe na sehemu za kuhifadhia na kuchakata samaki. Serikali iharakishe ununuzi wa meli na siyo kwamba isubirie ujenzi utakapokamilika ndipo inunue meli. *TAFICO*

inayo nafasi ya kununua meli nyingi zaidi kwa kutumia ubia kwa sababu mazingira ya uwekezaji tayari yatakuwa yametengenezwa, yatakuwa yamevutia na hii itasaidia kwa wawekezaji kuja kuwekeza katika bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na bahari kuu, maziwa makuu na mito mingi, nchi yetu bado haiko katika nchi tano ambazo zinafanya uvuvi wa kutumia vizimba. Bado haiongozi, iko nyuma, tunashindwa hata na nchi ya Kenya yenye ziwa peke yake, inatushinda katika uvuvi wa kutumia vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba pamoja na juhudi zinazofanywa na Wizara ya Mifugo ya kuwezesha watu wetu kufanya ufugaji wa vizimba basi wasimamie kuwe na tija zaidi kwa sababu hata nchini bado tuna upungufu mkubwa wa zao la samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Leah Komanya.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa muda wetu umefikia mwishoni, lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu nimeongeza dakika chache tumalizie wachangiaji wawili.

Kwa hiyo, namuita Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, atafuatiwa na mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Mohamed Issa.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu, nami niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan,

Makamu wa Rais - Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri Mkuu - Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Naibu Waziri Mkuu - Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko pamoja na wasaidizi wao wote kwa namna wanavyoshirikiana na kuhakikisha Serikali inafanya kazi kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wetu wa Fedha Mheshimiwa Lameck Mwigulu Nchemba, pamoja na Naibu Waziri wake na Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Kitila Mkumbo pamoja na Naibu Waziri wake, pia Makatibu Wakuu wao wa Wizara zote mbili kwa ushirikiano mkubwa ambao wametupatia kwenye Kamati yetu ya Bajeti. Naomba waongeze ushirikiano huo kwa Kamati nyinginezo pia pindi wanapohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutekeleza na kukamilisha miradi yake mikubwa hasa ya kielelezo na kimkakati. Tumeona mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere sasa liko kwenye kukamilika na hata hivyo, tumeona matunda yake. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kukamilisha ujenzi wa reli ya *SGR,* kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma. Wananchi tumeona matunda yake na tunayashuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Rais kwa ahadi yake alipokuwa ziarani Mkoani Ruvuma ambapo aliahidi atajenga reli ya kutoka Bandari ya Mtwara hadi Bandari ya Mbamba Bay. Ujenzi wa reli hiyo utasaidia kuinua uchumi wa wananchi wa mikoa inayopitiwa na ujenzi huo, ikiwemo Mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Njombe na maeneo mengine ya jirani. Ujenzi wa reli hiyo utapunguza uharibifu wa barabara unaofanywa na malori ya makaa ya mawe na pia utaondoa uharibifu na msongamano wa magari maeneo ya mijini. Vilevile utapunguza ajali, ikiwemo eneo la Songea Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye eneo la ulipaji wa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma. Kwenye ukurasa wa 59 wa Taarifa ya Kamati umeeleza, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hadi Juni, 2023 jumla ya madeni yaliyohakikiwa yalikuwa ni shilingi trilioni 3.3 na kiasi cha madeni ambayo hayajahakikiwa ni shilingi bilioni 64.7. Hata hivyo,

Serikali haijabainisha endapo madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ndio ambayo hayakuhakikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili naomba nilizungumze hivi, ziko baadhi ya taasisi zetu za Serikali, hasa upande wa halmashauri, tuna kawaida ya kuanzisha miradi mipya kila mwaka wa fedha unapoanza, wataalamu pale wanaanza na mradi mpya. Anaangalia faida yake yeye, kamisheni, yaani *ten percent* mradi mpya unapoanza maana atapata chochote ule mradi ukianza, bila kujali kuna fedha ambayo itasaidia kukamilisha mradi ule au laa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, kama tumeamua kuweka kwenye mwongozo naomba tuzingatie, tuusimamie mwongozo ule. Ni vyema tukakamilisha kwanza madeni yetu ya wakandarasi na watoa huduma wetu wote wa nyuma, tukifanya hivyo, watakuwa na ari mpya ya kuendeleza miradi ile ambayo wameianza. Wakandarasi wengi wameacha kufanya kazi kwa sababu wanaidai Serikali na siyo kwamba Serikali inadaiwa Hapana, ni wataalamu wetu ndiyo wanasababisha haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukijipanga Wakurugenzi hawa ambao wako kwenye zile halmashauri hakuna kuhama mpaka mradi wako ukamilike. Hawatahamishwa, wakikamilisha yale maana yake ndiyo wahamishwe, lakini kama Mkurugenzi atahamishwa pale anaacha mradi kiporo, Mkurugenzi anayekuja anaanza na mradi wake, hiyo siyo sawa. Mipango yetu hatuwezi kwenda nayo kwa mtindo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano kwenye baadhi ya mikoa ambako hata mimi nimeona na nimepitapita. Watalaamu wetu wengi wanapenda kumrubuni Mkurugenzi. Mkurugenzi kuna mradi huu hapa unatarajia kutekelezwa kwa fedha kidogo tu, tutafute fedha, tutapata fedha nyingine, wakati huo analenga faida yake yeye. Hiyo siyo sawa, tunawaumiza wakandarasi wetu. Tumeona wakandarasi wengi wamefilisika, wengine wamekufa kwa kuidai Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme Serikali hii haidaiwi yenyewe kama Serikali, wanaosababisha ni wataalamu wetu. Naomba wataalamu wetu huko kwenye halmashauri muionee huruma Serikali. Serikali haina fedha ya kuweza kutekeleza miradi kila tunapoibua tu mradi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kama tumeamua kutekeleza miradi viporo kwa awamu hii, twende na utaratibu huu. Tuanze kulipa madeni yote ya wakandarasi, tukishakamilisha twende kwenye miradi viporo, ile miradi viporo hatuwezi tu kwenda kusema tunatekeleza miradi viporo ni lazima tufanye tathmini. Tathmini ile kama itaundwa kamati kimkoa au kiwilaya ikatambua miradi iliyopo kwenye lile eneo maana yake iainishwe na ipangiwe bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kuna miradi mingine kwa mfano, miradi ya barabara, imetekelezwa mwaka juzi wameweka vifusi barabara imejengwa. Haya mvua imepita, barabara imeenda na maji, tunapoenda kukagua au kuhakiki hayo madeni, tukienda kuangalia hiyo barabara tunakuta nyasi zimeota, pale tutakuta barabara? Huyu mzabuni au mkandarasi tutamlipaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali tuwe *serious* na hili kama tumeamua kulipa madeni ya wakandarasi na watoa huduma. Tulipe hayo madeni na kama tumeamua ku…

*(Hapa kipaza sauti kilikata mawasiliano)*

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo nimalizie.

**MWENYEKITI:** Ahsante, naomba u-*wind up.* Malizia.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumeamua kukamilisha hiyo miradi viporo, naomba tukamilishe kweli miradi viporo na baada ya kukamilisha hayo, ndipo tuanze na miradi mipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka kwa mchango wako. Nimuite sasa Mheshimiwa Mohamed Issa, mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu, ili aweze kutoa mchango wake.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Mpango huu wa mwaka 2025/2026. Nimejaribu kusoma Mpango huu, hotuba zote nimeona ni nzuri na zinatupeleka pale ambapo Watanzania wengi watakuwa na matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye vipaumbele kuna vipaumbele vitano ambavyo ni kuendeleza miundombinu, kusimamia huduma za jamii, mazingira na tabianchi, usimamizi wa utawala bora na kugharamia uchaguzi wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa ningetamani ingekuwepo pia kusimamia na kuimarisha biashara za ndani na nje, sikuiona katika kipaumbele, hayo ndiyo maisha ya watu. Tumeona kwamba hizi zote zinakwenda katika Serikali, katika utoaji wa huduma kwa wananchi, ni jambo jema sana, lakini biashara ndiyo ambazo zinawafanya wananchi wanakuwa na fedha mifukoni ambazo zinawasababisha kuwa na umaliziaji wa mahitaji yao kama chakula na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nilitamani sana liwepo katika kipaumbele chetu katika mpango huu. Sasa tukisema biashara, nilitamani kwamba sehemu zetu za Wamachinga hawa zipewe kipaumbele na siyo kama hivi tunavyofanya sasa hivi. Tunawajengea Wamachinga nje ya mji matokeo yake wanakimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoa mfano pale Kariakoo, nchi nyingi tunavyokwenda hatukuti vurugu kama zile, lakini katikati ya nchi, katikati ya mji, unakuta kuna *mall* kubwa sana la Wamachinga peke yao ambalo linaweza kwenda ghorofa kumi na kwa upana, zaidi ya ekari mbili. Utakuta kwamba

wameingizana humo wanafanya biashara na watu wanakwenda maalumu kwa ajili ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunawatoa nje, jambo hili nilitamani Serikali ilipe kipaumbele. Mfano mzuri ni pale Kariakoo, sasa hivi tunajenga majumba yale, kwa nini tusichukue nyumba hata 20 tukajenga hiyo *mall* kubwa wakaingizwa Wamachinga, naamini wasingefanya vurugu na kila mtu angetamani kwenda Kariakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwenye suala la kuimarisha TEHAMA kwa ajili ya makusanyo ya nchi. Mimi nilitamani Bodi ya *TTB,* hawa *TTB* na watu wa maliasili wawe ndiyo *pilot* wetu kwa sababu wenyewe kwenye Ripoti ya *CAG* kule wamesema hawajaanza na wataanza. Sasa wawe *pilot* kwa sababu mapato makubwa hapa yanapotea, sasa TEHAMA ikaanzie huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kipaumbele cha mwisho, kugharamia uchaguzi wa mwaka 2025. Zanzibar kule kulitokea mauaji kwenye uchaguzi na mwanzo wake ulianzia kwenye gharama za uchaguzi, sababu kubwa ilikuwa ni uchaguzi wa mara mbili. Sasa sisi kama Wazanzibar hatuhitaji uchaguzi wa mara mbili, uchaguzi uwe ni wa pamoja na kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliopiga mwanzo walikuwa ni Watendaji wa Sekta za Muungano na kwa hiyo, bila shaka Serikali ya Muungano inahusika na hili. Kwa hiyo, tunahitaji tufanye uchaguzi, usiwe na malalamiko na usiliingizie Taifa hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nitachangia kwenye suala la *connection* ya umeme. Mimi siku zote nimekuwa nikichangia suala la umeme, kutenganisha mijini na vijijini katika *connection fees,* hili si muumini nalo kwa sababu wananchi hata kule mjini kuna maskini wengi na hawana uwezo, lakini hata *connection* kwa sehemu za mijini ni rahisi kwa sababu ukiutoa nyumba hii unaingia nyumba hii, lakini vijijini ni lazima unapata nguzo mbili, tatu, gharama ni kubwa. Sasa wanapokuja na mpango wao, wanapokuja kwenye bajeti, wamshauri Mheshimiwa Rais naye

alikubali hili kwa sababu yeye ndiye walimweleza, wakamdanganya Mheshimiwa Rais, akakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunavyohitaji ni kwamba wananchi wote *connection fee* hii iwe moja, kwa sababu *tariff* za umeme ndiyo zinaweza kurudisha gharama za *connection,* siyo hii *connection*. Wananchi wa mijini sasa hivi hawana umeme, unakuta nyumba tano, sita, ambao gharama zake ni ndogo. Kwa hiyo, ushauri wangu ni huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ni suala la afya; suala la afya bado tunalichezea, tumepitisha Sheria hapa ya Bima ya Afya kwa Wote tunaimba, lakini utekelezaji wake haufanyiki, mwisho tunasikia utafanyika mwaka 2026. Wananchi wanaumia, sasa hivi wanakufa, hawaendi hospitali kwa sababu hawamudu gharama za kwenda hospitali. Kila siku tunapiga *blabla* tu, leo mara unasikia sijui kuna kongamano, kuna nini, lakini hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka bima ya afya ya wote na ambayo kila mtu ambaye atakuwa amekata huduma hii, basi apatiwe, siyo kuchagua aina ya magonjwa. Jambo hili si zuri na halikubaliki, tunahitaji anayeumwa kansa atibiwe, anayeumwa figo atibiwe, tuna anayeumwa homa atibiwe, mwisho Watanzania wote wawe na afya njema na bora na wawe wazalishaji mali wanaoipenda nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Issa.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa wachangiaji wetu. Nawashukuru sana watu wote waliopata nafasi ya kuchangia siku ya leo, ili kuishauri Serikali kwa mujibu wa taratibu na sheria zetu.

Baada ya kusema hayo, Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Bunge linarudia.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza shughuli zetu za leo na ninaomba mnisikilize kwa makini, naahirisha Bunge hili mpaka kesho, tarehe 6 Novemba, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.17 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 6 Novemba, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*